Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatano Novemba 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581495
nipasheTZ nipasheTZ
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com



UKURASA 22
TEN HAG AKINGIWA KIFUA UTD

# Mvua yasababisha vifo watu watano

• **Idadi** yatarajiwa kuongezeka, Kamanda, madiwani walonga... *Ukurasa 2*





Mwonekano wa baadhi ya nyumba zilizoanza kubomolewa na maji ya Bonde la Mto Msimbazi, eneo la Tabata, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha. **Picha ndogo:** Mkazi wa eneo hilo, Baltazar Joseph, akionyesha nyumba yake ilivyobomolewa. **PICHA: JENIFER GILLA**

## Watumishi watatu wasimamishwa kazi 'utata' kifo cha mjamzito

UKURASA 3

**Hofu waishio mabondeni kusombwa na mafuriko**
UKURASA 5

UKURASA WA 2
**Dk.** Mwinyi awafariji waliokumbwa na maafa



UKURASA WA 3
**Waathirika** wa majitope wataka mil. 1.8/- badala nyumba ya mil. 20/-



UKURASA WA 5
**Wasanii** watumiaji, wahamasishaji dawa kulevya kikaangoni

**MICHEZO** SIMBA KWA CHASAMBI, YANGA CHIVAVIRO UK.24

**KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikabidhi cheti cha shukrani kwa Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), James Mlowe kwa udhamini wa mfuko huo, katika Mkutano wa 7 wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) mjini Lindi, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mvua yasababisha vifo vya watu watano

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha limeopoa miili mitano ya watu waliopoteza maisha kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia Novemba 13, mwaka huu, jijini Arusha.

Akizungumza jana baada ya kuopoa miili hiyo katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Arusha, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salvas Makweli, alisema baadhi ya miili hiyo bado haijatambuliwa na kwamba wanaendelea kufuatilia ili kufahamu majina yao kamili, umri na makazi yao.

"Hadi sasa (jana) tumeopoa miili mitano ukiwamo mmoja wa mwanamke na wanaume wanne. Miongoni mwao wametambulika kuwa ni Living Shirima (30), Ally Abdi na Wilson Rajabu wote wakazi wa jiji la Arusha.

"Miili iliyoopolewa imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mount Meru. Niwaombe wananchi ambao wana ndugu ambao hawakurudi nyumbani usiku wa kuamkia Novemba 13 mwaka huu, wafike hospitali ya Mount Meru kwa ajili ya kuangalia kama kuna ndugu yao aliyepoteza maisha,"alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Makweli, bado kazi ya uokozi inaendelea katika maeneo mbalimbali kadiri wanavyopata taarifa kutoka kwa wananchi.

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Arusha, Osward Manjejele, alisema mbali na miili hiyo pia watu sita wameokolewa wakiwa hai. "Mbali na maiti hizo tano, pia tumefanikiwa kuwaokoa watu sita usiku wa saa 7:00 katika maeneo mbalimbali, lakini niwaombe wana Arusha wachukue tahadhari wenyewe kwa maisha yao hasa wanaoishi mabondeni," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alisema madhara ni makubwa na wameanza ziara maalum inayoshirikisha kamati ya maafa na ile ya ulinzi na usalama kwa ajili ya kutembelea maeneo yote ya jiji kuainisha madhara ya mafuriko hayo.

"Madhara ni makubwa kwa kweli na tuko kwenye ziara kutembelea maeneo yote na kuainisha ili angalau waathirika wapate msaada ikiwamo kuopoa miili iliyosombwa na maji na iliyoko kwenye nyumba zilizojaa maji lakini pia kuangalia namna ya kuwasaidia wananchi kupata malazi na kuwahamisha wale walioko kwenye hatari zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Mtahengerwa, maeneo yaliyoathirika zaidi na mafuriko hayo ni kata za Muriet, Terrat, Majengo, Elerai, Sombetini na eneo la kwa Mrombo ambayo yanasababishwa na maji mengi ya mvua yanayotoka Arumeru kwenda maeneo hayo ambayo yamesababisha baadhi ya barabara kuharibika vibaya.

"Mbali na mvua lakini maji mengi yametoka Arumeru na hadi sasa madhara ni makubwa katika kata hizo. Tusubiri hadi baadaye tukikamilisha zoezi tutatoa taarifa. Kikubwa wananchi wawe watulivu na wasikivu, waaminifu pia utiifu katika zoezi hili tunalolifanya,"alisema.

Wakizungumzia madhara hayo, Diwani wa Muriet, Francis Mbise, alisema katika kata yake, miili mitatu ya watu imeshaopolewa kwenye mitaro na nyumba 23 zimepata madhara mbalimbali, ikiwamo kuingiliwa maji na kubomoka kuta huku baadhi ya maduka, vitu vikisombwa na maji.

"Barabara zimekatika zikiwamo za changarawe na hata za lami kutokana na mvua hiyo kubwa ambayo imesababisha pia vifo, baadhi ya nyumba kuharibika pamoja na barabara kukatika,"alisema.

Diwani wa Sokoni One, Michael Kivuyo, alisema madhara makubwa ya mafuriko hayo mbali na mwili wa mtu mmoja kuokotwa eneo la Lolovono, bado hawajapata idadi kamili kutokana na mti mkubwa kuziba daraja la kuelekea makazi ya watu.

"Madhara ni makubwa sana. Barabara zimejaa makorongo makubwa, madaraja yamejaa maji na vivuko. Hakufai, hofu kubwa ni baadhi ya nyumba zilizojaa maji kama wahusika wamenusurika hasa watoto, hivyo tunatafuta msaada wa kuondoa miti iliyoziba daraja la Uswahili tukaone hali ikoje huko kwenye makazi," alisema.

Diwani wa Ngarenaro, Isaya Doita, alisema madhara makubwa yaliyobainika hadi sasa ni nyumba kuangukia kuta na maduka kuvunjika zaidi ya 25 na vitu kusombwa na maji vikiwamo vibanda vya matunda na mboga pamoja na vyombo vya moto, hasa bodaboda waliokuwa wanadharau wingi wa maji.

"Baadhi ya vivuko vimekatika huku daraja kubwa la 'Kambi ya fisi' likivunjika na kukatisha mawasiliano kati ya Kata za Ngarenaro na Sakina,"alisema.

Mwaisha Abdul, mkazi wa eneo la Majengo Chini, alisema tangu juzi usiku wa manane, mvua iliponyesha, nyumba zilijaa maji na walikuwa wanapiga simu kuomba msaada kwa diwani wa kata yao ya Sombetini, Bakari Msangi, lakini alikuwa hapokei simu.

"Maji yote yanayotoka Arumeru yameelekezwa huku na vigogo walojenga jirani na barabara kubwa ya Arusha-Manyara hali iliyosababisha hadi makuburi kufukuliwa na tuna shaka miili iliyozikwa hivi karibuni, imezolewa na maji kwa sababu tumekuta sanda na makaburi yakiwa kama korongo," alisema.

Mmoja wa wananchi jijini Arusha, Rehema Swai, alisema kuwa hofu nyingine ni baadhi ya wanafunzi wa kidato cha nne ambao walistahili kufanya mitihani kuwa katika wakati mgumu. Alisema kutokana na mafuriko hayo na madhara ya mvua, huenda baadhi wasiende shuleni kufanya mitihani.

"Tunaomba serikali ikiwezekana iwasaidie baadhi ya wanafunzi walioshindwa kwenda shuleni kufanya mtihani wa kidato cha nne kutokana na mafuriko," alisema.

Neema Laizer, mkazi wa Kwa Mrombo, alisema mvua hiyo iliyoanza kwa kasi majira ya saa 1:00 usiku, imeezua zaidi ya nyumba 30, kusomba vyombo vya moto na bidhaa mbalimbali madukani.

## Rais Mwinyi awafariji watu waliokumbwa na maafa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewatembelea waathirika wa maafa ya mvua huku akisema serikali inatafuta ufumbuzi wa kudumu wa kuondokana na maafa yatokanayo na mvua kila zinaponyesha.

Dk. Mwinyi alitembelea maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mjini Magharibi yaliyoathiriwa na mvua na kutaja miongoni mwa njia za kutatua changamoto hiyo kuwa ni ujenzi wa miundombinu ya madaraja na mitaro ya kupitisha maji.

Alitaja hatua zingine zitakazochukuliwa na serikali ni pamoja na kuyasarifu maji ya mvua ili kutumika kwa shughuli mbalimbali.

Rais Mwinyi alisema lengo ni kuhakikisha wananchi hawapati maafa ya kuingiliwa na maji katika nyumba zao kila msimu wa mvua unapokuja.

Pia alisema kila msimu wa mvua kubwa, Zanzibar imekuwa ikipata mafuriko kutokana na kutokuwapo kwa miundombinu madhubuti ya kupitisha maji.

"Katika maeneo mengi niliyotembelea tatizo ni mitaro ama haipo au iliyokuwapo imeziba haipitishi maji vizuri, hivyo tutatafuta ufumbuzi wa kudumu ili tusije tena kutoa pole kila zinapotokea mvua kubwa," alisisitiza.

Rais Mwinyi alibainisha miongoni mwa sababu ya mitaro iliyopo kutopitisha maji vizuri ni kutokana na kuzidiwa na taka na kuwataka wananchi kutotupa uchafu katika mitaro hiyo ambayo imejengwa kwa gharama.

Dk. Mwinyi alionya taasisi zinazotoa vibali vya ujenzi ikiwamo manispaa na Wizara ya Ardhi kuacha kuvitoa katika maeneo hatarishi ikiwamo mabondeni.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema mitaro iliyopo ilizidiwa kutokana na kasi kubwa ya maji.

Aliahidi kuwa watakaa na watu wa mazingira na Mamlaka ya maji Zanzibar (ZAWA) ili kuona namna bora ya maji hayo kuyafanyia utaratibu mwingine yasiathiri wananchi.

Waziri Hamza alisema upo mpango kwa baadhi ya maeneo ya wananchi waliojenga, lazima wahamishwe ikiwamo maeneo ya mabondeni ili kupunguza athari.

Aliyataja baadhi ya maeneo hayo ni Fuoni Kibondemzungu, Tomondo Ziwa Maboga ambayo asili yake ni kutuwama maji mengi na ni ya wazi ambayo hayaruhusiwi shughuli za ujenzi.

Alisema ipo ripoti ya kitaalamu iliyofanywa na wanajiolojia inayoonesha kuwa, ardhi ya Zanzibar maeneo ambayo yapo wazi ambapo hayatakiwi kujengwa nyumba za ghorofa.

Baadhi ya wananchi walioathirika na mvua hizo walisema pamoja na serikali kujenga mitaro ya kupitishia maji ya mvua, lakini haijapunguza athari ya maji kuingia katika nyumba zao.

Nyumba 5,113 Zanzibar zimeathirika kutokana na Mvua kubwa zilizonyesha hivi karibuni ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ndiyo Mkoa ulioathrika zaidi na maafa hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkunde (wapili kulia), akiangalia bwawa jipya la kuhifadhia majitope katika Mgodi wa Almasi Mwadui wilayani humo, mkoani Shinyanga juzi, alipofanya ziara katika mgodi huo. Mkuu huyo, aliagiza bwawa hilo liwe linafanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara ili lisije bomoka na kuleta madhara kwa wananchi. Kulia ni Mhandisi Mkuu wa Mgodi huo, Shagembe Mipawa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Watatu wasimamishwa madai ya kifo mjamzito

**Na Waandishi Wetu**

TUKIO lenye 'utata' linalohusu tuhuma za kusababisha kifo cha mjamzito, Mariam Zahoro (39), baada ya kufikishwa Kituo cha Afya cha Kabuku, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, limewasimamisha kazi watumishi watatu kupisha uchunguzi wa sakata hilo.

Wakati tukio hilo likitokea Handeni, wajawazito wanaokadiriwa 100 kila mwezi hujifungulia kwa tochi ya simu kijiji cha Kiganila, wilayani Morogoro.

Katika tukio la Handeni, inadaiwa kuwa Mariam alifariki dunia akiwa hospitalini hapo baada ya kukosekana Sh. 150,000 za upasuaji.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Omari Mkangama, Novemba 13 mwaka huu, kifo hicho kilitokea Novemba 11, Kituo cha Afya Kabuku, ambako mama huyo alikuwa akipatiwa huduma.

Kutokana na tukio hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, imewasimamisha kazi watumishi watatu walioshiriki kumpatia huduma mama huyo hadi umauti ulipomkuta ili kupisha uchunguzi kupitia tume huru na bodi za kitaaluma.

Taarifa hiyo ilisema, Mkangama ameeleza ikibainika kuna uzembe ulifanyika hadi kusababisha kifo hicho, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao.

"Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mariam Zahoro Mohamed.

...Tunapenda kusisitiza kuwa huduma zote za afya kwa makundi maalum ikiwamo wajawazito ni bure."

**UMMY ATOA SIKU SABA**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ametoa maelekezo kwa Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT), na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC), ndani ya siku saba wampelekee taarifa ya kifo cha mjamzito na kichanga chake.

Alisema tayari hatua za awali zimeshachukuliwa ikiwamo ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, kutuma timu kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa mkoa, inayojumuisha madaktari bingwa wawili, akiwamo Daktari Bingwa wa wanawake na uzazi na Daktari Bingwa wa huduma za usingizi ili kufanya uchunguzi wa tukio hilo.

"Hatua nyingine iliyochukuliwa baada ya tukio hilo ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kuwasimamisha kazi watumishi watatu walioshiriki kumpatia huduma mama huyo, tangu alipopokewa kituoni hadi umauti ulipomkuta ili kupisha uchunguzi wa tukio hili baya na lisilopaswa kuvumiliwa," alisema Ummy.

Pia, Waziri Ummy amewahakikishia Watanzania kuwa baada ya kupokea taarifa ya uchunguzi, kila mtumishi aliyehusika atachukuliwa hatua kali za kitaaluma, kiutumishi na kijinai, ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alitoa pole kwa familia iliyoguswa na msiba huo na kuahidi kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya, itaendelea kusimamia ubora wa huduma za afya ili kufikia matarajio ya wananchi wote.

**WAJIFUNGUA KWA TOCHI ZA SIMU**

Wajawazito takribani 100 kila mwezi wanalazimika kujifungua kwa kutumia tochi ya simu katika zahanati ya kijiji ya Kiganila, Kata ya Selembala, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Akizungumza katika mkutano wa Baraza la Madiwani kupitia taarifa za kata robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/24, halmashauri ya wilaya hiyo, Diwani wa Kata ya Selembala, Msafiri Gilla, alisema wajawazito hao wanajifungulia kwa tochi kutokana na zahanati hiyo kukosa huduma ya umeme tangu mwaka 2021.

Alisema zahanati hiyo iliyojengwa mwaka 2017 kwa ufadhili wa wahisani ilikuwa ikitumia umeme wa jua, lakini baadaye mitambo iliharibika na kushindwa kufanya kazi.

Alisema, mwaka 2021 waliwasilisha maombi ya kijiji hicho kupatiwa umeme wa mradi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), lakini mpaka sasa zahanati hiyo haijapatiwa umeme licha ya kijiji hicho kufikiwa na umeme huo.

"Kitu cha kushangaza REA imefikisha umeme kwenye Kijiji cha Kiganila na tunawashukuru sana, lakini kwenye zahanati mpaka sasa kinamama wanajifungua kwa tochi, nimekuwa nikilisema sana hili tatizo katika baraza hili na leo narudia tena kwakuwa kiongozi wa REA yupo hapa tunaomba mtusaidie," alisema Diwani Gilla.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Lucas Lemomo, alisema ni muhimu maeneo yanayotoa huduma za kijamii yakapewa kipaumbile.

Alisema halmashauri ya wilaya hiyo imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kujenga zahanati pamoja na vituo vya afya ili wananchi wapate huduma bora za afya.

Mwakilishi wa REA, Hilary Kuchapa, akijibu hoja ya diwani ya zahanati kukosekana huduma ya umeme, alisema suala hilo analifikisha kwenye kikao cha juu ili liweze kupatiwa ufumbuzi wa haraka kwa kuwa yeye sio mtoa maamuzi.

* **Imeandaliwa na Godfrey Mushi (HANDENI) na Ashton Balaigwa (MOROGORO).**

# Waathirika wa majitope wataka mil. 1.8/- badala nyumba ya mil. 20/-

**Na Marco Maduhu,**
KISHAPU

WAATHIRIKA wanne kati ya 47 waliopoteza makazi kutokana na kubomoka kwa kingo za bwawa la kuhifadhia majitope katika Mgodi wa Almasi Mwadui, Kishapu mkoani Shinyanga, wamegoma kujengewa nyumba zenye gharama ya Sh. milioni 20 kila moja na kutaka wapewe Sh. milioni 1.8 kila mmoja.

Nyumba hizo zinazojengwa na mgodi huo kwa ajili ya fidia kwa wananchi hao, zinagharimu Sh. milioni 20 lakini kwa tathimini iliyofanyika, zilizoharibiwa zina thamani ya Sh. milioni 1.8 kutokana na kuwa za tope.

Mpaka sasa, hatua ya kufidia waathirika imefikia asilimia 99.6 na tayari wananchi 43 wamejengewa nyumba za kisasa ikiwa ni pamoja na kuhamisha makaburi 14 huku asilimia iliyosalia ni kwa wale waliogoma kujengewa nyumba.

Ofisa Uhusiano wa Mgodi wa Almasi Mwadui, Benard Mihayo, akizungumza wakati wa ziara ya kamati ya maafa ya tukio hilo, alisema watu hao wameomba kupewa fidia ya fedha taslimu ili wakafanye shughuli zao binafsi.

"Katika ulipaji fidia kwa kujenga nyumba 47, watu wanne wamegoma wakitaka wapewe pesa. Bado tunaendelea na mazungumzo nao ili kuwashawishi tuwajengee nyumba sababu ukiangalia tathimini ya fidia ya nyumba zao kiwango cha fedha ni kama Sh. milioni 1.8 ambacho huwezi kujenga nyumba," alisema.

Watu hao, akiwamo mwekezaji mmoja ambaye ni mchimbaji wa almasi katika eneo hilo, alisema yeye si mkazi wa eneo hilo, hivyo asingehitaji nyumba bali apatiwe fidia ya fedha taslimu aendelee na shughuli zake.

Mihayo alisema nyumba hizo 43 ambazo zimejengwa kilometa 20 nje ya eneo yalipotokea maafa hayo, ujenzi wake umefikia asilimia 91.4 na uko katika hatua ya umaliziaji. Alisema hadi kufikia Desemba, mwaka huu, zitakuwa zimekamilika na waathirika hao watakabidhiwa.

Pia aliwataka wananchi ambao bado wanasita kukubali kujengewa nyumba, wafanye uamuzi mapema bila kushawishiwa kwa kuwa endapo mgodi huo utaamua kuwalipa kwa mujibu wa tathimini ya nyumba zao, fedha zitakuwa ndogo na hazitawasaidia.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, aliupongeza mgodi huo kwa kushirikiana vyema na serikali kwa hatua zote tangu maafa yalipotokea na hadi sasa wako kwenye hatua za mwisho za ukamilishaji wa kulipa fidia wananchi.

Aliwataka wananchi wanne ambao wamegoma kujengewa nyumba wakitaka walipwe fidia ya fedha, kukubali kujengewa nyumba ili waishi mahali salama na kuendelea na maisha yao kama kawaida.

Aidha, aliusisitiza mgodi katika bwawa jipya la kuhifadhia majitope, wawe wanalifanyia ukaguzi wa mara kwa mara ili liendelee kuwa imara.

Mhandisi Mkuu wa Mgodi wa Almasi Mwadui, Shagembe Mipawa, kwa niaba ya Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Ayoub Mwenda, alisema katika janga hilo la kupasuka bwawa, waliathirika wananchi 304.

Baadhi ya wananchi ambao wamejengewa nyumba, walishukuru na kubainisha kwamba awali walikuwa wakiishi kwenye nyumba za tope lakini sasa wataishi kwenye nyumba imara za matofali ya saruji ambazo hawakuwa na uwezo wa kuzijenga.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
15.11.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **18.11.2023 hadi 23.11.2023** kampuni ya C**EVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga kuelekea Bandari ya Dar Es Salaam**, gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.5** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam kupitia Barabara ya Morogoro,** Barabara ya Mandela gari litasafiri muda wa mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117712402



Priscilla Chassama, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mashujaa wa Sikoseli Tanzania, akitoa ufafanuzi kuhusu ugonjwa huo jijini Mwanza hivi karibuni.**PICHA:NEEMA EMMANUEL**

# Selimundu; janga jipya afya nchini - 2

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

**TOLEO la jana la ripoti hii, lilieleza kila siku watoto 39 wanazaliwa wakiwa na ugonjwa wa selimundu nchini. Kati yao, 28 (asilimia 72) huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa huku Mkoa wa Mwanza pekee ukiwa na wastani wa watoto watano kwa siku. Endelea kujua madaktari wanasema nini.**

**MASHUJAA WA SELIMUNDU**

PRISCILLA Chassam, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mashujaa wa Sikoseli Tanzania, anasema wamejikita kutoa elimu katika jamii baada ya kuona ugonjwa huo unaenea kwa kasi kutokana na ukosefu wa elimu.

"Kumekuwa na migogoro kwenye familia. Mtoto akipatikana na sikoseli, lawama zinamwangukia mama, anatelekezewa familia na mtoto analelewa katika mazingira yasiyo salama pasipo kuelewa kuwa wazazi wote wanachagia kupatikana ugonjwa huo, hivyo wanapaswa kushirikiana wote katika malezi," anasema.

Anasema ni wakati mwafaka kwa jamii kuwa na tabia ya kufuata huduma sahihi za afya kwa mtu mwenye tatizo hilo. Kuwafungia ndani au/na kuwapeleka kwa waganga wa kienyeji wagonja wa selimundu ni kuhatarisha maisha yao.

"Tutaendelea kutoa elimu kwenye jamii ili kupunguza vifo vitokanavyo na sikoseli. Mpaka sasa tunatoa huduma kwa watu zaidi ya 300. Serikali itafute namna ya kufanya kampeni kwenye jamii hasa vijijini na kuhakikisha elimu juu ya sikoseli inawafikia wananchi ipasavyo.

"Kwa baadhi ya wilaya za vijijini tatizo ni kubwa. Mfano, tulikwenda Busega, walipimwa watu 365, nusu yao walikuwa na ugonjwa ya sikoseli, wengine wana chembechembe na wachache wakiwa hawana chembechembe wala sikoseli, Hapo utaona jinsi gani ugonjwa huo ulivyo mkali. Tunaendelea kutafuta fedha kuyafikia maeneo mengine ya vijijini," anasema.

**MADAKTARI BINGWA**

Daktari Bingwa wa Magojwa ya Watoto na Mtaalamu wa Selimundu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Emmanuela Ambrose, anabainisha kuwa tatizo la ugonjwa huo ni kubwa nchini.

Bingwa huyo anabainisha kuwa utafiti unaonesha asilimia 75 ya watoto wanaozaliwa na sikoseli duniani wanatoka Afrika. Tanzania ni nchi ya tano duniani na ya nne Afrika kwa tatizo hilo, sasa inao wagonjwa takribani 14,000 waliozaliwa na ugonjwa huo na wengi wao wakitokea Ukanda wa Ziwa Victoria.

Dk. Emmanuela anafafanua kuwa hospitali hiyo kwa sasa ina zaidi ya watoto 1,000 ambao wanahudhuria kliniki kwa mwaka. Kila Jumatatu wanawaona watoto 30 hadi 50 huku Ijumaa wakiwaona watoto 50 hadi 80.

"Tunatoa ushauri na kuwaelimisha wazazi na walezi kuwa ugonjwa wa sikoseli hurithiwa kutoka kwa wazazi wote wawili; baba na mama. Elimu zaidi hutolewa kwa jamii jinsi ya kuepuka kupata mtoto mwenye tatizo hilo.

"Utafiti zaidi unahitajika ili kueleza bayana ukubwa wa tatizo hili kwani ugonjwa huo kwa sasa umekuwa mada kubwa kwa sababu watoto wengi wanazaliwa wakiwa na shida hiyo. Tatizo hili ni kubwa kwa sasa kutokana na watu kutokuelewa wamerithi chembechembe za ugonjwa huo, wanatambua tu pale wanapopata mtoto mwenye shida hiyo.

"Kusubiri mpaka upate mtoto ni kuchelewa, wanapaswa watambue hali zao kabla ya kubeba ujauzito. Kama wote wana urithi wa sikoseli wafanye uamuzi mapema, hivyo ni vyema wakapima kabla ya kuingia kwenye ndoa.

"Pia mtoto anapozaliwa apimwe, akikutwa na tatizo hilo anaanzishiwa kliniki na matibabu ya sikoseli mapema ambayo yatamsaidia kutibu matatizo yote yanayotokana na ugonjwa huo, hivyo kumfanya kuishi muda mrefu," bingwa huyo anashauri.

Njia nyingine ya kukabiliana na ugonjwa huo, Dk. Emmanuela anashauri mama mjamzito anapoanza kilinki apimwe hali yake, akionekana amebeba chembechembe iandikwe kwenye kadi yake ya cliniki 'AS' (ana chembechembe za selimundu), 'SS' ( ana selimundu) na AA (mtu asiyekuwa na chembechembe wala sikoseli).

"Watoto wote watakaozaliwa na mama mwenye SS au AS, lazima wapimwe hali zao watakapozaliwa. Hiyo itasaidia kuondokana na ugonjwa huu. Kupima watoto wote pia kutasaidia kupunguza gharama kwa nchi kukabili ugonjwa huu," anashauri.

Bingwa huyo pia anashauri kuwe na somo mahususi la selimundu shuleni kuchochea jitihada za kukabili ugonjwa huo. Upimaji wa selimundu ufanyike hadi shuleni ili watoto wajue hali zao wakiwa wadogo. Itawasaidia kutambua hatari iliyoko mbele yao na watakuwa makini.

Dk. Emmanuela anaweka wazi kuwa matibabu ya selimundu ni ghali, akiutaja ni ugonjwa wa kudumu. Mzazi lazima awe na fedha na hasa kwa wale walio juu ya miaka mitano.

Anafafanua kuwa muda mfupi baada ya kuzaliwa, mtoto akigundulika ana ugonjwa huo, anaanzishiwa dozi ya Folic acid inayosaidia uzalishaji damu. Pia dozi ya Penicillin V inayozuia magonjwa yanayosababisha vifo hasa kwa watoto chini ya miaka mitano na anapofikisha umri wa miezi tisa wanahakikisha ameanza dozi ya Hydroxyurea.

Dk. Emmanuela anasema anatamani serikali isaidie kutoa dawa kwa wagonjwa hasa dozi ya Hydroxyurea inayosaidia kupunguza shida zinazotokana na sikoseli ikiwamo maumivu, kulazwa mara kwa mara kuongezwa damu na kuzuia kupata kiharusi (kupooza) na damu kuwa nyepesi.

"Kupandikiza uroto ndio tiba, lakini ni gharama sana. Pia lazima uroto huo utoke kwa ndugu yako unayeendana naye kibaiolojia. Hapa nchini ni watoto wanne tu wamefanyiwa na wote wako salama, lakini nina imani wengi zaidi watafanyiwa hasa ambao hydroxyurea haijawa msaada kwao," afafanua.

**KULIKONI KANDA YA ZIWA?**

Dk. Emmanuela anaeleza kuwa Kanda ya Ziwa ni moja ya kanda za kitopikia ambazo zina tatizo kubwa la malaria, akiwa na ufafanuzi kuwa mwili wa binadamu umeshabuni njia ya kupambana na malaria kwa kusababisha hitilafu katika vinasaba na kuleta urithi wa sikoseli.

"Kwa hitilafu hii warithi waliweza kuishi/kujikinga na ugonjwa wa malaria uliokuwa chanzo kikubwa cha vifo. Hitilafu hiyo ikirithiwa kutoka kwa wazazi wote wawili ndio huleta ugonjwa wa sikoseli. Kuoana wenyewe kwa wenyewe katika sehemu za kitopikia imekuwa ni chanzo cha ongezeko la ukubwa wa tatizo.

"Pia kwa sasa utandawazi, watu kusafiri na kuishi na kuchanganyika maeneo mengine kumefanya tatizo la sikoseli kuwa sehemu nyingi nchini na duniani.

"Ndoa za mitala ndizo zinaleta urithi, sikoseli na Ukanda wa Kitopikia hasa Mwanza. Kitu cha muhimu ni kufanya vipimo kabla ya kuoana na ikibainika mna urithi wa sikoseli, bora msioane ili kuepuka nafasi ya kupata mtoto mwenye ugonjwa wa sikoseli," anashauri.

Hoja ya kuepuka kuoana wenye urithi wa sikoseli, inaungwa mkono na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Kansa kwa Watoto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Shakilu Jumanne, anayesema kuwa licha ya mikakati mingi ya kupunguza makali ya ugonjwa huo, hali ni mbaya nchini.

Anasema watoto wengi wanaendelea kuteseka na ugonjwa huo kutokana na uelewa mdogo wa wazazi kuhusu namna ya kuepuka mazingira yanayoweza kuchochea seli nyekundu kubadilika umbo na kuwa mundu.

Kama ilivyotolewa angalizo na mtangulizi wake Dk. Emmanuela, Dk. Jumanne pia alitahadharisha ndoa za watu wenye vinasaba vyenye ugonjwa huo zinachochea watoto kuzaliwa na ugonjwa wa sikoseli kwa sababu wote wanakuwa na vichocheo vya kurithi.

"Kila mwaka hapa nchini watoto 14,000 huzaliwa na ugonjwa huu huku watoto 10,000 kati yao huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mkoa wa Mwanza tu wanazaliwa watoto 1,700 kwa mwaka wenye tatizo hili," anatahadharisha.

Takwimu hizo zina maana kwamba, kila siku watoto 39 wanazaliwa wakiwa na ugonjwa wa selimundu nchini. Kati yao, 28 (asilimia 72) huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa huku Mkoa wa Mwanza pekee ukiwa na wastani wa watoto watano kwa siku.

Kuhusu matibabu ya ugonjwa huo, Dk. Jummanne anaungana na Dk. Emmanuela kwamba njia ya ukakika zaidi ni kupandikiza uroto kutoka kwa ndugu wa karibu kwenda kwa mtoto mwenye tatizo.

"Matibabu ya sikoseli ni ghali hususani katika kupandikiza uroto. Huduma hii kwa mgonjwa mmoja hugharimu Sh. milioni 30 hadi 40, jambo ambalo ni gumu kwa Watanzania wenye maisha duni.

"Hivyo, ili kuepuka haya, lazima jamii ikubaliane kupima kabla ya ndoa ili kuwaepusha watoto wetu maumivu wanayopitia," bingwa huyo anashauri.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sikoseli Wizara ya Afya, Dk. Asteria Mpoto, anabainisha kuwa serikali inafanya jitihada kuweka unafuu kwenye huduma za sikoseli ikiwa ni pamoja na kuimarisha matibabu ya kibingwa ya kupandikiza uroto.

Anabainisha kuwa kwa kuanzia, serikali imeanza kugharamia matibabu ya kibingwa kwa watoto wenye ugonjwa huo kwa kupandikiza uroto ili kuwapunguzia maumivu wanayoyapata.

# Hofu waishio mabondeni kusombwa na mafuriko

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI athari za mafuriko zikiendelea katika maeneo mbalimbali nchini, wananchi wengi wanaokumbwa na adha hiyo, wana mengi ya kusimulia, yakiwamo hofu ya vifo, kupoteza mali zao na watoto kukosa masomo na maisha ya kukesha usiku.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini hali hiyo inatawala kila ifikapo msimu wa masika au mvua nyingi kama za El Nino. Pia shughuli za kiuchumi husimama, wanandoa kutawanyika, kila mmoja akitafuta pa kujistiri kwa namna yake.

Mkazi wa Mtaa wa Msimbazi Mama, Tabata, Ilala, jijini Dar es Salaam, Baltaza Joseph, alibainisha alivyonusurika kufa baada ya ukuta wa nyumba yake kuanguka wakiwa wamelala ndani na familia yake.

Alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa 7:00 usiku wakiwa wamelala bila wasiwasi na kwamba walishtushwa na kelele za majirani zilizoashiria kuwa nyumba inaanguka.

"Tulisikia majirani wakipiga kelele nyumba inaanguka! Nyumba inaanguka! Nikaamka haraka na kumwamsha mke wangu nikamwambia tutoke nje haraka kuna nyumba inaanguka. Kumbe ilikuwa nyumba yetu sina habari," alisema.

Walipofungua mlango, alisema walishangaa kuona sehemu ya ukuta sebuleni uliokuwa upande wa Mto Msimbazi umeanguka, ndipo waliporudi ndani haraka na kuwabeba watoto na kukimbilia nje.

Alisema kitendo cha kutoka nje tu, ukuta wote ulioko upande wa mto huo ulianguka na kusababisha sakafu ya sebuleni nayo kumeguka na kuanguka hali iliyosababisha baadhi ya mali zilizokuwamo ndani kusombwa na maji.

Kutokana na tukio hilo, Joseph alisema alipoteza vitu vyake vya thamani vikiwamo TV, friji, kabati la vyombo, vitanda na magodoro huku akiachwa bila makazi, hali inayomlazimu kuomba hifadhi kwa jirani.

Joseph alisema hali hiyo licha ya kumwacha masikini, inamwathiri kisaikolojia kwa kuwa hakutarajia kuwa atakuja kukosa mahali pa kuishi na kuomba hifadhi kwa jirani.

Wahenga wanasema mwenzio akinyolewa tia maji. Hali hiyo ilimkuta pia jirani wa Joseph, Tamasina Raymond, ambaye alisema kwa sasa anaishi kwa wasiwasi akiamini kilichomtokea mwenzake, kitamtokea na yeye kwa mara ya pili.

Mwaka 2021, alisema alipatwa na mkasa kama huo baada ya mvua kubwa kusababisha mafuriko katika mto huo ambayo yalifika hadi kwenye nyumba yake na kubomoa ukuta.

Alisema alikwenda kupanga chumba kimoja ili ajisitiri na mtoto wake lakini alilazimika kurudi na kujenga chumba kimoja katika eneo hilo na kuendelea na maisha kwa kuwa hakuwa na uwezo wa kuendelea kupanga.

Kutokana na hali hiyo, anasema mvua zinaponyesha usiku, anakosa usingizi kwa kuhofia maji yanaweza kujaa na kusababisha madhara kama ilivyotokea awali.

Aliiomba serikali kuwatembelea na kuona namna ya kuwasaidia ikiwamo kujenga mawe pembezoni mwa ukuta wa mto huo ili kuzuia mmomonyoko wa udongo unaosababisha nyumba kubomoka pia kuwalipa fidia kama ilivyowaahidi ili watafute mahali pengine pa kwenda.

**ATHARI WATOTO**

Tatu Mohamed alisema kitendo cha kukesha usiku mvua zinaponyesha kinaathiri masomo ya watoto wake kwa sababu ifikapo asubuhi ndipo wanalala kufidia usingizi waliokosa kwa kukesha.

Alisema wanalazimika kukesha kwa sababu mara nyingi mvua zinaponyesha, huingia ndani na kusababisha uharibifu hasa kwenye vifaa vya umeme na magodoro.

Mohamed alisema mwaka 2021 mvua ilisababisha kupata hasara kwa kulowesha makochi, vitanda na magodoro huku friji na luninga vikiharibika kwa kuingia maji.

**KUKWEPA MAFURIKO**

Mkazi wa Mtaa wa Barabara ya Kawawa, Kinondoni Mkwajuni, Manipaa ya Kinondoni, Ramla Rashid, alisema kwa sasa hata mvua zikiingia ndani kwake haziharibu mali kwa sababu amegundua njia mpya ya kuviweka juu ya kichanja.

Alisema amejenga kichanja cha mbao katika sebule yake ambapo akiona kuna dalili ya mvua kubwa anaweka vitu vya thamani ikiwamo luninga, mafriji na magodoro ili visiingie maji.

"Huku sisi tumeishajulia hii mvua, tukiona maji yamevuka kwenye kingo ya ukuta wa daraja lile, tunajua hapa lazima yataingia ndani, tunapandisha mali zetu kwenye vichanja sisi tunaomba hifadhi nyumba za juu huko ," alisema

Akizungumza baada ya kukagua eneo la Jangwani juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, aliwaelekeza wakuu wa mikoa na wilaya nchi nzima kuwatembelea wananchi, kukagua athari za mvua na wasaidie wanaohitaji msaada.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alipozungumza na gazeti hili Novemba 12, mwaka huu, alisema serikali imeshapata fedha za ujenzi wa mradi wa DMPD awamu ya pili ambao utajenga barabara za mitaa kwa kiwango cha lami.

Alisema kwa eneo la Jangwani, tayari kuna mradi wa ujenzi wa daraja utaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 600 ambao utaboresha mfumo wa maji kupita kwa urahisi kwenda baharini.

Pia alisema wameshafanya tathmini na wakazi wanaoishi pembezoni mwa Mto Msimbazi watalipwa fidia ili wapishe ujenzi.




Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Jimbo la Ilala, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kuchambua miswada ya sheria kuhusu uchaguzi, tume ya uchaguzi na ya vyama ya siasa iliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasanii watumiaji dawa za kulevya kikaangoni

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania (DCEA), imesema ina orodha ya wasanii wanaotumia, wanaohamasisha kupitia nyimbo na mavazi, matumizi ya dawa za kulevya, huku akiwataka kuacha mara moja kwa kuwa mtambo wa utambuzi unakaribia kukamilika.

Aidha, amesema sheria inaipa mamlaka DCEA kupima mtu yeyote anayehisiwa kutumia dawa za kulevya, na kwamba mtambo maalum unaojengwa uko mbioni kukamilika na utakuwa na vifaa vya kisasa vya kutambua kiasi mtu alichotumia.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alisema hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili ya wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari kuhusu majukumu, uelewa kuhusu dawa za kulevya, sheria na nafasi ya vyombo vya habari nchini kupiga vita uingizwa na usambazaji wa dawa hizo.

"Ninawaonya wasanii wanaotumia dawa za kulevya, wanaohamasisha matumizi kupitia nyimbo zao na mavazi, tutawakamata na kuwapima kisha tutawapeleka mahakamani na iwapo watakutwa na hatia watakwenda jela miaka mitatu," alisema.

"Ninavyozungumza hapa vifaa tayari vipo bandarini, ni vya kisasa vina uwezo wa kutambua kiasi cha dawa alichotumia mtu. Wasanii wote watambue kuwa tuna orodha yao wanaotumia cocaine, heroin na bangi, tunawapa muda wa kujirekebisha vinginevyo hatua kali zitachukuliwa," alisema.

"Tunaangalia nyimbo zao, matendo yao, mavazi yao wanaonyesha namna wanavyohamasisha matumizi ya dawa za kulevya. Maabara ikikamilika tutawapima na baada ya hukumu tutawapa huduma maalum ya kuwatoa kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Tulishazungumza na BASATA na kuwakabidhi orodha ya wasanii husika, tuliwataka wajirekebishe, wasipofanya hivyo hatua zinafuata," alisema.

"Mamlaka haitaangalia ukubwa wa msanii, anapendwa kiasi gani wala ana nyimbo nzuri kiasi gani ilimradi mtambo umeonyesha anatumia dawa za kulevya basi kinachofuata ni kwenda mahakamani, hakimu akimkuta na hatia ni jela miaka mitatu."

Alisema wasanii ni kioo cha jamii, wana mashabiki na wafuatiliaji wengi wanapohamasisha jambo linafuatwa na wengi na kwamba kwa wanachokifanya kinahamasisha matumizi ya dawa za kulevya, kupitia nyimbo zao, matendo yao na wanapokuwa jukwaani, jambo ambalo siyo sahihi ni kuteketeza kizazi.

Kuhusu matumizi ya shisha, alisema sheria iko mbioni kukamilika na itauzwa katika maeneo maalum ambayo hayatafikiwa na wengi na kuondokana na kinachoendelea sasa kuuzwa na kutumiwa ovyo.

"Wanawake wengi wameingia kwenye matatizo kutokana na kuchanganyiwa dawa za kulevya kwenye shisha, ni kosa kisheria kuchanganya dawa za kulevya kwenye shisha, inatumiwa na watu wengi na udhibiti unakuja kutakuwa na mabadiliko makubwa," alisema.

Lyimo alisema wamekutana na vijana wa vyuo vikuu vya ndani na nje ambao wametumbukia kwenye dawa za kulevya kupitia makundi, ambayo hudanganyana kuwa kwa kutumia hiyo itawawezesha kusoma kwa muda mrefu, jambo ambalo siyo sawa kwa kuwa linawathiri kiakili na afya.

"Tuna mifano ya vijana walikwenda kusoma nje ya nchi wamerudi wamesha athiriwa na dawa za kulevya, kuna wengine wa vyuo vyetu vya ndani wanatumia, wengi wanadanganyana wanapata nguvu na uwezo wa kusoma zaidi na hivyo kufanya vizuri darasani jambo ambalo siyo sawa kwa kuwa madhara ya baadaye ni makubwa," alisema.

Kuhusu kuhalalisha bangi nchini, alisema hilo haliwezi kufanyika kwa kuwa madhara ni makubwa na nchi zilizoruhusu zimeweka utaratibu unaodhibitiwa, nyingi zinazokamatwa nchini zinatokana na nchi zinazozalisha kuzidiwa.

"Kilimo cha bangi hakiwezi kuruhusiwa nchini, tumeona nchi zilizoruhusu zimeshaelemewa, lakini hali ya usalama siyo ya kuridhisha, kuna ujasusi na vita kunakochangiwa na dawa za kulevya. Tanzania hatuwezi kufika huko. Tunawaonba wote wanaosimama kuhamasisha na kutaka kushinikiza kilimo hicho kuruhusiwa kuacha mara moja.

"Nchi haiwezi kuendeshwa kwa kutegemea uchumi wa bangi, wanaolima mbona hatuwaoni wakilima pareto, pamba au mazao mengine ya biashara, kwanini wanang'anga'ania bangi tu. Halafu anasimama mtu ambaye ana ushawishi kwenye jamii anataka turuhusu hili haliwezi kukubalika, hata Rais Samia Suluhu Hassan alishasema hatuwezi kuruhusu matumizi ya bangi."

Alisema madhara ya matumizi ya dawa za kulevya ni makubwa ikiwamo saratani ya utumbo, koo na kuathirika kwa mfumo wa hewa, wapo waliokuwa wanatumia wanajuta kufanya hivyo.

Alisema kumekuwa na kudanganyana kuwa dawa hizo zinaongeza nguvu za kiume na kusahau nguvu hizo ni kwa muda mfupi na zinaufanya mwili kufanyakazi zaidi ya uwezo wake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii isaidie kutoa ushahidi kupunguza ukatili kijinsia

**MOJA** ya tatizo linalokwamisha polisi kudhibiti wahalifu wa ukatili wa kijinsia ni jamii kukwepa kutoa ushahidi wa kuwatia hatiani watu wao.

Tatizo hili ni kubwa na hata jamii inaposhuhudia ukatili ukifanyika, hawako tayari kutoa ushirikiano kwa polisi.

Matokeo yake lawama huenda kwa jeshi la polisi likidaiwa kuwaachia wahalifu wa vitendo vya ukatili wakiendeleza kufanya vitendo hivyo.

Jamii pia inayopatwa na tatizo hilo, iko tayari kumaliza suala hilo nje ya vyombo vya sheria wengine kwa kuogopa aibu ikigundulika mwanafamilia amefanyiwa vitendo hivyo.

Hii sio sawa kabisa, kwa sababu jamii inapoendelea kukumbatia vitendo hivyo, wahalifu wanaendelea kuwaumiza wengine na wao kujiona wapo juu ya sheria.

Taarifa zinazotolewa kwenye madawati ya kijinsia ya polisi, zinaeleza kuwa vitendo hivyo vinazidi kuongezeka katika jamii na kutoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano wa kutoa ushahidi.

Kwa mfano dawati la jinsia la Jeshi la Polisi Chang'ombe, lilitoa takwimu zinazoonyesha kuwa kwa wiki moja hupokea takribani kesi 10 na miongoni mwa hizo nane hukosa ushahidi na watuhumiwa kushindwa kushughulikiwa na kuachiwa huru.

Aidha, matukio yanayoongoza kuripotiwa kwenye dawati hilo ni pamoja na ulawiti.

Matukio ya watoto kuharibiwa kwa kufanyiwa vitendo vya ukatili yanaumiza hasa kwa mzazi ambaye anategemea mtoto wake akue katika maadili mema na baadaye aweze kuwa kiongozi mzuri, anaharibiwa kisaikolojia na kupoteza mwelekeo wa maisha.

Wazazi wanajukumu kubwa la kuwafuatilia watoto wao na nyendo zao ili wanapowabaini kubadilika wawahoji na kugundua ili waweze kuchukua hatua mara moja.

Hata hivyo, wazazi wengine licha ya kujua watu wanaowaharibu watoto wao hubaki kimya na kufanya siri ili jamii isigundue kuwa mtoto wake amefanyiwa kitendo kibaya.

Kukaa kimya ni kuendelea kumuumiza mtoto na kumpa nguvu mhalifu kuendelea kuharibu watoto wengine ambao ni tegemeo la nguvu kazi ya baadaye.

Huu ni wakati wa kila mzazi/mlezi bila kujali mtoto umemzaa kushirikiana kuwataja wahalifu wote ili waweze kuchukuliwa hatua.

Kesi kama hizo zinapopelekwa kwenye Jeshi la polisi na kuomba jamii kutoa ushirikiano wa kutoa ushahidi ni vizuri wakajitokeza, bila kufanya hivyo, ushahidi utakosekana na wahalifu wataendelea kutamba mitaani wakiharibu watoto.

Jeshi la polisi linapata changamoto ya kukamilisha taratibu za kisheria kwa kuwa linakosa ushahidi kutoka kwa jamii.

Wanaharakati wa haki za binadamu na taasisi zinazotetea watoto, mara kwa mara zinatoa elimu kwa wananchi umuhimu wa kuwataja wahalifu wanaofanya vitendo vya ukatili ili viweze kudhibitiwa, lakini baadhi bado wanakumbatia.

Wazazi wengine wananyamazishwa kwa kupewa pesa na wahalifu ili wasiweze kwenda mbele ya sheria kushtaki na kwa sababu ya hali ngumu ya uchumi waliyonayo wanaona bora wachukue na kuziba mdomo.

Kama hali itaendelea hivyo, basi watoto wengi wataishia kuharibiwa na wahalifu na kuzima ndoto zao za kuwa taifa la vijana wenye nguvu.

Kutoa ushahidi unaposhuhudia kitendo cha uhalifu ni jambo muhimu sana kwasababu utaokoa vizazi vingi na kukomesha vitendo hivyo kuendelea katika jamii.

Ushirikiano ni jambo la msingi na siku zote wananchi huwa msaada mkubwa kwa jeshi la polisi kufanya kazi yake kwa urahisi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Restuta-James

# Ndoano haiwezi kumvua mamba

**JE**, mwaweza ninyi kudhibiti mchwa kwa kelele au kuziba mirija ya kuchepusha fedha za umma kwa maneno? Mmesahau mipango ya wizi aliyojiwekea kiongozi huyo asiyejali maisha bora kwa Mtanzania ndio fahari yake?

Huona sauti za umma kama kelele za chura hivyo mjadala wa wabunge hauwezi kumkimbiza.

Ninaporejea kishindo cha wabunge kukemea ubadhirifu wa mali ya umma unaoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, CAG hivi karibuni, najiuliza nini kitafuata?

Je, serikali itapeleka bungeni muswada kama baadhi ya wabunge walivyopendekeza? Au imefanikiwa kwa kiasi gani kudhibiti mchwa wa fedha za umma? Naelewa kwamba kuna tofauti kubwa ya mijadala ya mambo yanayohusu nchi kati ya awamu ya tano na hii ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan ambayo imeruhusu uhuru wa ukaguzi, wa kutoa maoni na michango ya wapinzani hata vyombo vya habari.

Mathalani, ripoti ya CAG, ya mwaka wa fedha 2021/22 iliweka bayana ubadhirifu na matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma kuanzia serikali kuu, tawala za mikoa na serikali za mitaa pamoja na mashirika ya umma.

Kasoro za ripoti hizo pamoja na zile zilizowahi kuibuliwa miaka ya nyuma na mapendekezo yake zinapaswa kuifanya mihimili ya dola kuanzia serikali,bunge na mahakama kuimarisha mifumo yote ili keki ya taifa inufaishe wananchi wengi zaidi.

Kuimarisha mifumo kutakomesha ubadhirifu ili Watanzania wanufaike na rasilimali za nchi.

Kwamba pamoja na juhudi nyingi za miradi ya kimkakati ya kiuchumi na kijamii inayoendelea, mifumo na taasisi imara za kusimamia mapato ya nchi zitasaidia kutokomeza maadui watatu waliotangazwa na Mwalimu Julius Nyerere, zama za uhuru mwaka 1961 ambao ni ujinga, maradhi na umaskini , na hata leo wanawatesa wananchi karibu kila mahali.

Hii ni kwa sababu katika kila ripoti za CAG, kumekuwepo na ubadhirifu wa fedha za umma unaotokana na sababu mbalimbali na mojawapo kubwa ni kutowajibika ipasavyo kwa wenye mamlaka ya kusimamia mapato na rasilimali za nchi kwa manufaa ya wengi.

Katika mjadala wa wiki iliyopita ambao baadhi ya wabunge walipendekeza itungwe sheria ya kunyonga wezi wa fedha za umma huku wengine wakipendekeza baadhi ya mawaziri waongoze jahazi kwa kupewa adhabu hiyo, umenifikirisha na kunishtua.

Wabunge wamepuuza kwa makusudi au kwa kutojua mapendekezo ya CAG kwa kuamua kudhibiti wezi wa kesho na kuwaacha ambao wameshatuibia na waliotuibia leo.

Kitendo hicho kinapingana na mapendekezo ya CAG kwenye ripoti ya ukaguzi ya mwaka jana aliyependekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuwachukulie hatua wabadhirifu wote wa fedha za umma na kutunga sheria kuhakikisha kila senti inayokusanywa kwenye Halmashauri inapelekwa benki kabla ya kutumika.

Swali la kujiuliza ni vipi halmashauri hutumia pesa mbichi (ambazo hazijaingizwa kwenye mifumo na kupangiwa matumizi)?

Je, bilioni 88.42 zilizotolewa kwenye vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu zinarejeshwaje? Tunaziacha zipotee kwa kutunga sheria ya kunyonga au tuikabe TAMISEMI iwawajibishe wahusika?

Kwa mtazamo wangu, mawazo ya wabunge yalipaswa kukabili mchwa wa jana na kuja na njia muafaka ya kuwadhibiti wajao.

Mbinu hiyo ni kuimarisha taasisi na mifumo ya nchi ili kila mlaji afahamu wazi adhabu ya kuchezea maisha ya wananchi. Wawakilishi wasisahau walaji hao wamehujumu shule ambazo hazina madarasa na madawati ya kutosha hivyo watoto wetu kurundikana darasani na kukaa chini, lakini pia ni chanzo cha miradi mingi kutokukamilika kwa wakati au isitekelezwe sababu serikali haina fedha za kulipa wakandarasi.

Wabunge wetu wamesahau kuwa watoto wengi wa walalahoi hawana fursa ya matibabu kutokana na kukosa bima ya afya ya toto afya kadi.

Aidha, wamesahau kuwa ubadhirifu umesababisha mbegu na mbolea ambavyo ni muhimu kwa kilimo kinachoajiri Watanzania wengi kupanda bei ilhali kama fedha zingekuwepo pengine ruzuku ingeongezeka zaidi na kuwapa wakulima nafuu.

Pia wamekisahau kilio wagonjwa kulala wane, mama wawili waliojifungua na watoto wao, kwenye kitanda kimoja hospitalini.

Wabunge na bunge linafahamu kuwa mchwa walipaswa kuogopa wanapojadiliwa bungeni na ikibidi waachie ngazi. Wezi wakemewe, wawajibishwe kwa kuchukuliwa hatua ikiwamo kuondolewa kwenye nyadhifa zao bila uonevu ili kuleta nidhamu ya matumizi ya serikali kwa kuboresha huduma muhimu za kijamii kama elimu, afya, maji na miundombinu.

HABARI KITAIFA

# Kamati ya Bunge yataka taasisi za serikali kulipa bili za maji

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge, Uwekezaji na Mitaji ya Umma, imeziagiza taasisi za serikali zilipe madeni ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) ili iweze kutoa huduma hiyo kwa wananchi wengi zaidi.

Kamati hiyo pia imeahidi kuendelea kuisaidia (DAWASA) kuishinikiza serikali kutoa fedha kwa mamlaka hiyo ili kusambaza huduma ya majisafi kwa wananchi wa maeneo yote ya Dar es Salaam na Pwani.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Deo Sanga, wakati wa ziara ya kutembelea utekelezaji wa mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu unaohusisha upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Wami.

Alisema DAWASA inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha huduma ya majisafi inapatikana kwa wananchi wote kwa kutumia mapato ya makusanyo ya ndani.

Vile vile, miongoni mwa maazimio ambayo kamati imetoa kwa serikali kwa ajili ya utekelezaji ni pamoja na kuhakikisha madeni ya taasisi zinazodaiwa na DAWASA yanalipwa ili kasi ya maboresho ya huduma za maji iendelee.

"Pia na madeni ya maji ya taasisi yaweze kulipwa ili kazi ya kusambaza maji kwa wananchi kupitia miradi mikubwa kama huu wa Chalinze awamu ya tatu iweze kuleta tija kwa wananchi, tunaipongeza Menejimenti ya DAWASA kwa jitihada kubwa wanazofanya za kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wote," alisema Mwenyekiti Sanga.

"Lengo la ziara ya Kamati hii ni kusimamia utekelezaji wa matumizi ya mitaji ya serikali kwa taasisi ili tija ya uwekezaji iweze kuonekana," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, aliishukuru Kamati kwa kutembelea na kujionea jitihada zinazofanywa na DAWASA kwa kushirikiana na mkoa katika kufanikisha azma ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani.

Alisema kwa sasa upatikanaji wa majisafi kwenye Mkoa wa Pwani ni asilimia 85, ongezeko linalovutia uwekezaji mkubwa wa viwanda.

Aliiomba Bunge kupitia kamati hiyo kuiwezesha DAWASA kupata fedha zaidi za kusambaza maji kwa wananchi wote wanufaika wa miradi.

Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete aliieleza Kamati kuhusu jitihada kubwa zilizofanywa na serikali kupitia DAWASA za kutekeleza mradi wa Chalinze awamu ya tatu pamoja na mradi wa maji Mlandizi - Chalinze – Mboga, ambao umekamilika na umeleta unafuu wa huduma ya maji.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, alisema mradi wa maji Chalinze ulipitia hatua mbalimbali za utekelezaji kuanzia awamu ya kwanza, ya pili na sasa awamu ya tatu ambayo inaendelea.

Alisema awamu hii ya tatu ambayo imegharimu Sh. bilioni 83, mradi unahusisha upanuzi wa uwezo wa mtambo wa Wami kutoka uzalishaji wa lita milioni 7.2 kwa siku hadi lita milioni 21.6.

Pia, mradi umehusisha ujenzi wa matangi 18 ya kuhifadhi maji pamoja na ujenzi wa vioski 351 vya kuchotea maji ambavyo tayari vimekamilika.

"Mradi umelaza bomba la usambazaji maji kwa umbali wa kilomita 826, na unalenga kunufaisha wakazi wa vijiji zaidi ya 56," alisema Kingu.



Mbunge wa Chalinze ambaye ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Utumishi, Ridhiwan Kikwete (wa tatu kushoto), akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Uwekezaji na Mitaji ya Umma, wakati walipotembelea utekelezaji wa mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu unaohusisha upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Wami, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Anayeshtakiwa kusafirisha vinyonga aongezewa kosa utakatishaji fedha

**Na Kulwa Mzee**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya Uhujumu Uchumi inayomkabili Eric Ayo na wenzake wanaodaiwa kukutwa na vinyonga 164, umebadili hati ya mashtaka na kumuongezea Eric shtaka la utakatishaji fedha.

Hati hiyo mpya ya mashtaka ilisomwa jana na Wakili wa Serikali, Cathbert Mbilinyi, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shahidi.

Wakili Mbilinyi aliwataja washtakiwa wengine katika kesi hiyo kuwa ni Ally Ringo na Aziz Ndago, ambao wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na nyara za serikali ikiwamo vinyonga 164 bila kibali. Akisoma hati mpya ya mashtaka, Wakili wa Serikali Mbilinyi alidai kati ya Desemba mosi, 2020 hadi Januari 20, 2021, washtakiwa hao waliongoza genge la uhalifu.

Alidai washtakiwa waliongoza genge la uhalifu katika mikoa ya Morogoro, Tanga na Dar es Salaam kwa kukusanya, kusafirisha na kuuza nyara za serikali ambazo ni vinyonga 164, nyoka sita na mijusi 20.

Imedaiwa katika tarehe na maeneo hayo, washtakiwa hao walijihusisha na nyara hizo za serikali bila kibali zenye thamani ya Sh. 20,789,730.

Mshtakiwa Ayo, anakabiliwa na shtaka la utakatishaji fedha na inadaiwa Januari 26, 2021 katika Benki ya CRDB Msamvu, Morogoro, mshtakiwa huyo alibadili Dola 400 kuwa fedha za Tanzania sawa na Sh. 923,600 huku akijua zilitokana na uuzaji wa nyara za serikali bila kibali.

Wakili Mbilinyi alidai upelelezi wa shauri umekamilika, aliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kuwasomea hoja za awali washtakiwa hao.

Hakimu alikubali ombi hilo na kuahirisha kesi hadi Novemba 28, mwaka huu. Washtakiwa hao waliachiwa kwa dhamana isipokuwa Ayo ambaye yuko mahabusu kwasababu shtaka la utakatishaji fedha halina dhamana.

# Akiri kortini kukutwa mifuko 24 ya salfeti yenye bangi

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Frank Mwita, amekiri kukutwa na mifuko ya salfeti 24 ikiwa na bangi na mbegu zake wakati akichukuliwa maelezo yake ya onyo na polisi na kudai kuwa bangi hizo huwa anazisafirisha kwa njia za malori hadi Dar es Salaam.

Aidha, imedaiwa kuwa Mwita alikuwa akinunua kiroba kimoja kwa Sh. 300,000, puli moja kwa Sh. 3,000 na kuwazuia watumiaji wadogo wadogo.

Hayo yalidaiwa jana na Wakili wa Serikali Winiwa Samson mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Evodia Kyaruzi wakati akisoma maelezo ya onyo ya mshtakiwa, baada ya kumaliza kusoma maelezo ya mashahidi saba katika kesi hiyo (Committal Proceedings). Alidai kuwa, mshtakiwa wakati anahojiwa na polisi alidai kuwa ni dereva, lakini kwa wakati huo (mwaka 2021) alikuwa hafanyi kazi hiyo na pia ni mzaliwa wa Butiama, mtoto wanne kuzaliwa.

Pia, alidai kuwa anafahamu kwamba anashtakiwa kwa kosa la bangi na alipoulizwa kama na yeye ni mvutaji, alidai kuwa ni mvutaji na wakati akiwa njiani alikamatwa na polisi.

"Polisi walipekua nyumbani wakakuta bangi mifuko ya salfeti 24, anakumbuka bangi hizo alikuwa akinunua kutoka kwa mtu mmoja anayemfahamu kwa jina la Manywele na Musoma bucha, anatumia kusafirisha mzigo kwa njia ya malori," alidai Mwita katika maelezo yake ya onyo.

Samson alidai kuwa wakati mshtakiwa alipohojiwa kuhusu wateja wake, alidai kuwa anawauzia watumiaji wadogo wadogo ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

"Nakumbuka kila kiroba nilikuwa nanunua kwa Sh. 300,000 na mimi na funga puli moja nauza kwa Sh. 3,000. Nafahamu kwamba ni kinyume cha sheria ila ugumu wa maisha ndiyo umenifanya nifanye biashara hii, haramu," alidai mshtakiwa katika maelezo yake.

Pia, mshtakiwa katika maelezo hayo alidai kazi hiyo ameifanya kwa muda wa mwaka mmoja na kuhusu kuwa na mzigo mkubwa kiasi hicho, alidai huwa anakusanya kidogo kidogo hadi unafikia wingi huo.

Hakimu Kyaruzi alimuuliza mshtakiwa kama ana chochote cha kuzungumza.

"Mheshimiwa Hakimu ninayo ya kuzungumza ila kwa sababu mahakama yako hii haina mamlaka ya kusikiliza kesi hii nitakwenda kuzungumzia mbele," alidai mshitakiwa Mwita.

Hakimu Kyaruzi alimweleza mshtakiwa kuwa mwenendo unachapwa na nakala la jalada la kumbukumbu, vikiwa tayari atapewa na pia hadi kikao cha mahakama kitakapopanga kesi yake ndiyo ataletwa mahakamani.


Mshitakiwa Mwita, alinyoosha kidole na hakimu alimpa nafasi ya kuzungumza.

"Mheshimiwa Hakimu kuna wengine kule gerezani wanalalamika kwamba ni mwezi watatu sasa tangu wasomewe committal proceedings hawajapata nakala, sasa na mimi si itakuwa kama wao," alidai Mwita. "Ahsante kwa kutupatia taarifa, karani utalishughulikia hilo, umesikia," aliagiza Hakimu Kyaruzi.

Ilidaiwa kuwa, Februari 25, 2021 mshtakiwa Mwita akiwa eneo la Kurasini, Kijiji cha Wavuvi Temeke, Dar es Salaam alikutwa akisafirisha bangi zenye uzito wa gramu 419.84.

Pia, alikutwa akisafirisha bangi yenye uzito wa gramu 19.61, 6.63 na 6.09 kinyume cha sheria, taarifa hizo polisi walipewa na msiri kuwa kuna mtu anauza bangi mtaani kwao.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Wanajiografia 250 kujadili fursa maendeleo ya kiuchumi, kijamii

**Na Restuta James**

ZAIDI ya wadau 259 wa mifumo ya kijiografia (GIS), wanatarajiwa kukutana kwa siku mbili kuanzia kesho ili kujadili na kuibua fursa zinazotokana na mifumo hiyo katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya RootGIS, Antidius Kawamala, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi kuwa watakaokutana ni wadau kutoka sekta ya umma na binafsi ambao wataeleza namna GIS inavyorahisisha utendaji wa kazi na ufanyaji biashara.

Alisema lengo ni kuelimisha umma kuhusu mifumo hiyo na namna watumiaji wanavyoweza kunufaisha wengine kwa kurekodi taarifa wanazopata.

"GIS ni mifumo ya kiramani inayowawezesha watu wa sekta zote kuanzia kilimo, tiba, usafiri, uvuvi, maji na nyinginezo kufahamu ni wapi wanaweza kupata mahitaji kulingana na wanachotafuta. Mfano mtu anaweza kuingia msituni na akapata mti wa tiba fulani, anachokifanya anapin (nakili) ile location (eneo), ili kumwezesha mtu mwingine kufika hapo kwa urahisi," alisema.

**Wadau hao wanatarajiwa kukutana jijini Dar es Salaam na mgeni rasmi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Tehama.**

Kawamala alisema kwenye kilimo, mifumo inasaidia kutunza kumbukumbu za shamba ikiwamo hali ya rutuba na unyevunyevu kwenye udongo.

Alisema wavuvi nao wanaweza kuitumia kwa kunakili eneo lenye samaki wengi ili waweze kuvua kwa urahisi siku zinazofuata.

Alifafanua kuwa washiriki watajifunza namna ya kutengeneza mifumo rafiki, ili wananchi wengi zaidi waweze kuitumia.

"Kwa mfano mamlaka za maji zinatumia GIS kujua mtandao wa mabomba yake...kwenye usafiri tunaona namna ambavyo mifumo hii inarahisisha kumpata dereva," alisema Kawamala.

Mwakilishi wa taasisi ya Youthmappers, Erick Mnyali, alisema wanafunzi wa vyuo watapata nafasi ya kujionea fursa za GIS na wanavyoweza kuongeza ubunifu ili kuiboresha.

Wadau hao wanatarajiwa kukutana jijini Dar es Salaam na mgeni rasmi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Tehama.

Kwa mujibu wa Kawamala, GIS inajumuisha muunganiko wa programu mbalimbali za kijiditali, watumiaji na takwimu.




Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Usalama Barabarani nchini, ACP Michael Deleli (wa tatu kulia), akitoa cheti kwa mmoja wa wanafunzi wa shule ya msingi Makuburi, walioshinda nafasi ya kwanza katika mashindano ya uchoraji wa picha ya 'Via Creative', yaliyoandaliwa kwa ushirikiano kati ya TotalEnergies Foundation, TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, East African Crude Oil Pipeline (EACOP) na Nafasi Art Space jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kwa lengo la kutoa mafunzo ya usalama barabarani kwa wanafunzi wa shule za msingi za Dar es Salaam na Bagamoyo. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Nafasi Art Space, Lilian Hypolite (wa tatu kulia), Mkuu wa Sheria, Mashirika, Rasilimali watu na Utawala wa TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Getrude Mpangile (wa nne kulia), Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Ellon Kamau (kulia) na Mwakilishi wa EACOP, Maria Mlay. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ushauri watolewa kudhibiti rushwa nchini

**Na Grace Gurisha**

BODI ya Ushauri ya Kupambana na Rushwa katika Umoja wa Afrika (AUABC), imesisitiza kuwekwa taratibu za kuwalazimisha viongozi wa serikali kuanzisha miundombinu ya kupambana na rushwa.

Mjumbe wa bodi hiyo, Kwami Senanu, alisema hayo kwa niaba ya Mwenyekiti wakati wa kuwakaribisha wajumbe wanne wapya, kwa lengo la kuimarisha AUABC kupambana na rushwa.

"AUABC hutumika kama msingi kwa nchi wanachama kuunda sheria zinazopinga vitendo haramu, kushughulikia kutokuwapo kwa sheria kama hizo katika nchi fulani," alisema Senanu.

Pia, alisisitiza umuhimu wa kukuza maadili kwa kufanya kazi kwa bidii, nidhamu binafsi, uaminifu, na uadilifu, hasa katika malezi ya watoto ili kupambana na rushwa.

"Wanachama wa AUABC, hasa wanne waliochaguliwa hivi karibuni, wanapaswa kuelewa kwamba utawala bora haupatikani kwa urahisi, lazima wajipange ili kuisaidia bodi," alisema. aliwataja wajumbe hao kuwa ni

Erica Ndlovu, Marthe Boulangar, Cheikh Ahmed na Abeba Menegste kutoka nchi ya Botswana, Ethiopia, Mouritania na Chad, pia mkutano huo ulilenga kuwaelekeza wanachama wapya na kuimarisha umuhimu wa kutekeleza majukumu yao.

"Dhamira ya AUABC ya kupambana na ufisadi na kuhakikisha kuwa uongozi hauchukuliwi kama biashara, bali ni kiini cha kweli cha uongozi wao," alisema Senanu.

Mmoja wa wajumbe hao, Principe Ntibasume kutoka nchini Burundi alisema kuwa wanakwenda kuufanyia kazi ushauri huo kwa kuchangia zaidi mapambano dhidi ya rushwa na kujifunza kutoka kwa wengine ili kufanya vizuri zaidi.

alisema kuwa rushwa ni jambo la kimataifa na ni hatari kwa maendeleo ya nchi yoyote, lakini changamoto ni mbaya zaidi barani Afrika na mahususi kwa Afrika, ni wajibu wa kila mtu kukusanya pamoja vita dhidi ya rushwa na ni kikwazo katika kuipiga vita.

# COSTECH yazindua kitabu kusaidia watafiti, wabunifu

**Na Sabato Kasika**

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa ushirikiano na watu wa Sweden na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), wamezindua kitabu cha kongano bunifu kitakachowasaidia wabunifu na watafiti kufanikisha zaidi ubunifu na bidhaa zao sokoni.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa (COSTECH) Dk. Amos Nungu, alisema kitabu hicho kinaongelea masuala ya kongano ubunifu, wakishirikiana na wenzao wa Sweden na SIDO.

"Kuandikwa kwa kitabu hiki ni sehemu ya majukumu ya COSTECH, katika kuwafikia wananchi, kushirikiana nao na kutatua changamoto zilizopo kwenye jamii, hasa katika ubunifu," alisema Dk. Nungu.

Aidha, alisema kwenye kongano bunifu wanasaidia makundi ya watu mbalimbali kukutana pamoja na kutatua changamoto walizo nazo, kitabu hicho kimeandikwa kama sehemu ya waliojifunza.

"Pamoja na wadau tunaoshirikiana nao, wapo watu kutoka vyuo vikuu, kwani ni moja ya washiriki waliofanikiwa kupeleka wanafunzi wao katika kongano zetu kufanya utafiti," alisema.

Dk. Nungu alifafanua kuwa kitabu hicho kwa sasa kipo katika lugha ya Kiingereza baadaye kitakuwa katika lugha ya Kiswahili ili ujumbe uliokusudiwa uwafikie watu wengi katika jamii kujifunza mengi kuhusiana na kongano.

Mmoja wa waandishi wa kitabu hicho kutoka COSTECH, Meneja wa upatikanaji na uendelezaji wa teknolojia, Dk. Athumani Mgumia, alisema COSTECH inajivuna kutengeneza mwongozo, ambao unaonyesha jinsi watu wanavyoweza wakafanya ubunifu endelevu.

"Lengo la COSTECH ni kusaidia wabunifu na kuratibu ubunifu, tumeandika kitabu hiki ili tukutanishe watu hawa pamoja tuweze kujua teknolojia zinazozalishwa na watafiti ziweze kutumiwa na wajasiriamali kufanya bidhaa zao ziwe shindani sokoni," alisema Dk. Mgumia.

Alisema changamoto iliopo ni wabunifu na watafiti hawawezi kufanya kazi pamoja, wengine wanafanya sayansi, huku wengine wakifanya biashara na kupitia mwongozo huo waliozindua ni kuweka mazingira ili watafiti na wabunifu waweze kukaa pamoja.



## RC atoa siku tatu AUWSA, Jiji kurekebisha miundombinu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella ametoa siku tatu kwa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (AUWSA), Jiji la Arusha, kurekebisha miundombinu ya barabara zilizoharibiwa na mvua kulikosababishwa na mamlaka hiyo kupitisha mabomba kwenye barabara na kumwaga kifusi bila kushindilia.

Mvua hiyo iliyonyesha usiku wa kuamkia Novemba 13 mwaka huu, kuanzia majira ya saa moja usiku na kusababisha baadhi ya mitaro, vivuko, madaraja, barabara kuvunjika na nyumba za baadhi ya wananchi kujaa maji na kukosa makazi.

Mongella, alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea eneo la Msasani lililopo Kata ya Murieti jijini Arusha na kukutaka barabara ikiwa imetitia na magari kuzama, kutokana na AUWSA kuchimbua barabara hiyo na kupitisha mabomba ya maji na kuacha bila kufukia vizuri

"Kaimu Mkurugenzi, mhandisi wa AUWSA John Ndetico ninakupa siku tatu mlete kifusi hapa pamoja na mtambo wa kushindilia, kwa sababu usanii mlioufanya hapa wakati mnapitisha mabomba wa kumwaga kifusi bila kushindilia, ndiyo umesababisha athari zote hizi za barabara hii kufungwa na watoto kushindwa kwenda shule.

"Kazi hii ianze sasa ya kuchimbua barabara hii, kuweka kifusi, kushindilia kwa kutumia mtambo ili ndani ya siku tatu kazi hii iwe imemalizika. Kila siku asubuhi nitapitia hapa kabla ya kwenda ofisini, kuona jinsi ambavyo kazi inaendelea. Sasa nyie nendeni mkalale ofisini halafu nije nikute hakuna kilichofanyika, muone ni nini kitatokea,"alisema.

Kadhalika, Mongella aliagiza AUWSA, kuhakikisha kuwa inafanya marekebisho ya kina kwa kuweka kifusi na kushindilia kwenye barabara zote ambazo walipitisha mabomba na hawakuzitengeneza kwa kiwango kinachotakiwa kama walivyozikuta awali.

Katika hatua nyingine, Mongella aliwataka wananchi wa Mkoa wa Arusha, kuchukua tahadhari za kina kipindi hiki cha mvua, ikiwa ni pamoja na malezi ya watoto ili kuepuka kusombwa na mafuriko au mali zao kuharibiwa.

"Bado mvua zinaendelea kunyesha kwa wingi kama tuluvyotangaziwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa. Rai yangu kwa wananchi wa mkoa wetu, tuchukue tahadhari ikiwa ni pamoja na kuangalia usalama wa watoto wetu, hasa wakati wa kwenda shule, mvua zikiwa zinanyesha ili kuepeuka madhara yasiyo ya lazima," alisema.

Pia, aliagiza AUWSA kukagua maeneo yote waliyopitisha miundombinu hiyo ya maji taka, iliyoharibu barabara na kutengeneza upya kwa viwango vinavyotakiwa na kusisitiza kuwa atapita kila siku kwenye maeneo hayo usiku na mchana kukagua iwapo marekebisho yanafanyiwa kazi.

Katika hatua nyingine Mongella aliiagiza AUWSA kushirikiana na wenyenviti wa mitaa, wakati wa kufanya marekebisho hayo na kuacha tabia ya kutowashirikisha kwa kigezo kuwa ni wana siasa.

"Mhandisi Ndetico wakati mnarekebisha hizi barabara wenyeviti wa mitaa husika, washirikishwe asije akatokea mtu huko akasema mwenyeviti ni wana siasa. Tusije tukalaumiana baadaye.

"Wazazi na walezi muwe makini kuangalia watoto wenu wasije kuzama maana barabara zimetitia, muwe makini ili maafa mengine yasije tokea,"alisema.

Mhandisi Ndetico, alisema amepokea maelekezo yote yaliyotolewa na Mongella na watayafanyia kazi, japo mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi huo, kampuni kutoka China ya Sinohydro Corporation Ltd alishamaliza muda wake.

Awali, Mwenyekiti wa Mtaa wa Msasani, Rashid Chidi alisema wakati AUWSA wanaweka miundombinu ya maji taka waliwaeleza changamoto ya barabara kuharibika, lakini waliambiwa waache kuingiza siasa katika masuala ya utaalamu.

"Hapa hali ni tete wananchi hawezi kutoka barabara zimeharibika vibaya magari yamezama, lakini kibaya zaidi wananchi wanashindwa hata kutoka majumbani kutokana na makorongo makubwa kwenye barabara na tunahofia watu wakikanyaga, waweza kutitia kwa kuwa ina nyufa kila mahali, na watoto wetu wameshindwa kwenda shule.

# Kamati: Kiwanda cha ngozi Kilimanjaro kuongeza ajira

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, imeridhishwa na maendeleo ya mradi wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro, ikieleza kukamilika kwake kutachochea upatikanaji wa ajira na kuondokana na uagizaji wa viatu visivyo na ubora nje ya nchi.

Kiwanda hicho kinamilikiwa kwa asilimia 86 na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), na Jeshi la Magereza linamiliki asilimia 14.

Akizungumza jana, baada ya kukagua kiwanda hicho katika Manispaa ya Moshi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia kwa dhati dhana ya uchumi wa viwanda.

Alisema kuwa soko la ndani la viatu kama litakuwa kubwa, uagizaji kutoka nje ya nchi wa viatu vyenye ubora wa chini nao utapungua.

"Tutaishauri serikali kuendelea kuweka fedha za kutosha kuhakikisha uzalishaji unakuwa endelevu. Tunaposema tunaelekea uchumi wa viwanda miongoni mwa viwanda vitakavyokuwa bora Afrika kiwe ni kiwanda hiki nchi za SADC (Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika), Jumuiya ya Afrika Mashariki ziagize kutoka hapa kuongeza upatikanaji wa ajira," alisema.

Mjumbe wa kamati hiyo, Almasi Maige na Neema Lugangira, kwa nyakati tofauti, wameipongeza serikali kwa uwekezaji huo na kushauri kujitangaza na kupanua wigo wa upatikanaji wa wateja wa makundi mbalimbali kutokana na ubora wa viatu hivyo.

Baada ya ukaguzi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliahidi serikali itaendelea kufanyia kazi ushauri wa kamati kwa kuwa kipaumbele kikubwa cha Rais Samia ni kuleta ustawi wa Watanzania.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Patrobas Katambi alisema soko la viatu limeendelea kuimarika na kwa sasa kuna taasisi nyingi za serikali zinachukua huku mikakati ikiendelea kuhamasisha taasisi zingine kuchangamkia viatu hivyo ambavyo vina ubora unaotakiwa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, aliieleza kamati hiyo kuwa gharama ya uwekezaji wa mradi huo hadi utakapokamilika inakadiriwa kufikia Sh.bilioni 152.96.

Kwa mujibu wa Kashimba, mradi huo unatarajiwa kurudisha gharama zake ndani ya miaka 10, kuanzia pale mradi utakapokamilika.



Katibu Tawala mkoa wa Tanga, Pili Mnyema (katikati) akijadiliana jambo na Katibu Tawala wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Jumaa Mhina, baada ya kumaliza kikao cha kusikiliza kero za watumishi wa kada zote wa halmashauri hiyo, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# New Zealand kuendelea kufadhili mradi wa FtMA

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI ya New Zealand imekubali kuendelea kutoa ufadhili wa miaka mitatu wa Mradi wa Farm to Market Alliance (FtMA), unaolenga kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya mahindi, alizeti, maharage na mpunga katika Mkoa wa Manyara.

Jana, Ofisa wa Wizara ya Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Gaye Readivys, alitoa ahadi hiyo baada ya kuridhishwa na usimamizi wa watendaji wa Shirika la Farm Africa, Vyama vya Ushirika wa Mazao (AMCOS) na taasisi za utafiti.

Radivys, alitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya kilimo katika AMCOS za Mbungwe, Matufa na Muungano.

Ofisa huyo aliuliza maswali juu ya mbegu wanazotumia, pembejeo na mashamba wanayomiliki, ili kujiridhisha kama wanazalisha kwa tija na kupata kipato.

Mratibu wa mradi huo katika Mkoa wa Manyara, Thomas Mmbaga, alisema mradi unatekelezwa wilaya za Babati, Hanang', Kiteto na Simanjiro.

Mmbaga alisema mradi ulianza Aprili 22 mwaka jana, na unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Norway (NORARD) na kusimamiwa na jumuisho la mashirika sita ambayo ni Shirika la Chakula Duniani (WFP), Agra, Yara, Syngenta, Bayer na Rabobank. Aidha, alisema lengo la mradi huo ni kuongeza uzalishaji kwa wakulima wadogo kwa kuwapatia fursa za masoko kupitia vituo vya kutoa huduma za kilimo kwa wakulima katika kata na vijiji na kuongeza kipato cha kaya.

Alisema kwa Manyara, mradi unafanya kazi na vituo vya kutolea huduma 89 zikiwemo AMCOS 30, wauzaji wa pembejeo 20, vikundi vya wakulima 23, wakulima viongozi watano, wachakataji wa mazao tisa na vyama vya kuweka na kukopa mbili.

Alitaja kazi zilizofanyika kuwa ni utoaji wa elimu na mafunzo, masoko na kutengeneza mtandao wa kibiashara kati ya vituo vya kutolea huduma kwa wakulima na wadau wanaojihusisha kwenye mnyororo wa mazao ya kilimo.

Mmbaga, alisema mazao yote yaliyokusanywa ni kilogramu 20,354. 50 na kiasi kilichouzwa ni kilogramu 7,232.57 na kuwaingizia fedha wanachama Sh. bil. 10. 139.

Akieleza uzoefu wao, Katibu wa Mbungwe AMCOS, Ernest Morembwa, alisema wameweza kuunganishwa na masoko ya uhakika akitolea mfano zao la alizeti kuuza kilogramu moja Sh. 1,200 wakati awali walikuwa wanauza kilogramu moja Sh. 600.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Bodi ya Mbungwe AMCOS, Teresia Wilbroad, alisema kupitia mradi huo na Farm Africa, wameunganishwa na vituo vya utafiti na kujua namna ya kuzalisha mbegu na sasa wanazalisha mbegu bora za ufuta na kuuza kwa wahitaji.





# Serikali yajipanga kudhibiti migogoro ya ardhi vijijini

**Na Alex Sayi,** MASWA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii imeeleza dhamira ya serikali kupitia mradi wa uboreshaji usalama wa miliki za ardhi vijijini kuhakikisha inadhibiti migogoro ya ardhi vijijini pamoja na kupunguza ujenzi wa makazi holela.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Timotheo Mzava ambaye pia ni Mbunge wa Korogwe Vijijini wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara kufuatia ziara iliyofanya wilayani Maswa mkoani Simiyu, iliyolenga kuona utekelezaji wa mradi huo.

Alisema kuwa utekelezaji wa mradi huo utawasaidia wakazi wa wilayani hapa huku akitaja utekelezaji wake utasaidia kuondoa migogoro kati ya kijiji na kijiji, shamba na shamba, kiwanja na kiwanja na kuongeza thamani ya ardhi na kuwasaidia wananchi kuboresha maisha yao.

"Tumefika hapa kujionea utekelezaji wa mradi huu, tumejionea na tumeridhika ombi letu kwenu ni kuwa msikiuke makubaliano ya mipaka mliojiwekea mkifanya hivyo gharama zilizotumika kutekeleza mradi huu hazitakuwa na maana tena,"alisema Mzava.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, Geofrey Pinda alisema kuwa Wilaya ya Maswa ni miongoni mwa wilaya saba za awali zinazonufaika na utekelezaji wa mradi huo ikiwemo Mufindi, Songwe, Mbinga, Chamwino, Longido na Tanganyika.

Pinda aliongeza kuwa vijiji vilivyoingizwa kwenye mpango ni 106 kati ya hivyo 120, huku vijiji vitano kati ya 120 vikitarajiwa kupandashwa hadhi na kuhamishiwa kwenye Halmashauri ya Mji wa Maswa na vijiji tisa vinapandishwa hadhi na kuwa miji midogo

"Mradi umeainisha hekta 77,664 na zimeshatambuliwa kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji, hekta 481 zimetengwa kwa ajili ya uendelezaji wa taasisi mbalimbali ikiwemo shule, makanisa na maeneo yakuzikia na hekta 713 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda," alisema Pinda.

Mkuu wa Idara ya Ardhi wilayani hapa, Vivian Christian alisema kuwa mradi huo unatekelezwa kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka 2022 hadi 2027 kwa gharama ya Sh.bilioni tatu na ulianza Februari, 2023 ambapo mpaka kufikia Novemba, 2023 umetumia Sh. milioni 819.

Aliongeza kuwa mradi unajumlisha shughuli za kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, upimaji wa vijiji 106 kuandaa mpango wa matumizi ya vijiji hivyo, utambuzi, upimaji wa mashamba na utoaji wa hati miliki za kimila 100,000.




Meneja wa Mkondo wa chini wa gesi asilia PanAfrican Energy Tanzania (PAET), Mhandisi Sabas Oisso (kushoto) akiwa na Meneja Mkazi wa TAQA Dalbit nchini, Amr AbouShady (katikati) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Primefuels Africa, Nikesh Mehta, katika uzinduzi wa kituo kipya cha kujaza gesi asilia cha TAQA Dalbit jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC awatangazia vita wazazi wanaokatisha masomo wanafunzi

**Na Remmy Moka,** SAUT

MKUU wa Wilaya ya Misungwi, Paul Chacha ametangaza vita dhidi ya wazazi wanaokatisha masomo ya watoto wao kwa lengo la kutaka waolewe au kufanya kazi za nyumbani wakisingizia ugumu wa maisha.

Alitoa kauli hiyo juzi baada ya mwanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari Sumbugu iliyopo wilayani hapa, Anastasia Mathias kutoroshwa na mama yake Monica Kazimini.

Inaelezwa kuwa mama huyo alimtorosha binti yake na kumpeleka mkoani Kagera kwa lengo la kufanya kazi za ndani, huku hali ambayo ingesababisha mtoto huyo kutokufanya mtihani wake wa mwisho.

"Baada ya upelelezi tulibaini kuwa mtoto amepelekwa Biharamulo kwa ajili ya kufanya kazi za ndani bila kujali kuwa alitakiwa afanye mtihani, lakini hata hivyo tulifanikiwa kumrejesha ili afanye mtihani wake tulimshikilia mama yake na hatua za kisheria dhidi yake zitaendelea hapo baadaye," alisema Chacha.

Aidha, alieleza katika mtihani uliopita wa kidato cha pili walifanya tathimini na kubaini kuwa zaidi ya wanafunzi 105 katika wilaya hiyo hawakufanya mitihani hiyo na kuwataka wazazi kuheshimu suala la elimu na umuhimu wake kwa watoto wao.

Vilevile, alieleza kuwa baada ya mtihani ya kidato cha nne kumalizika itafanyika tathmini ya kutambua idadi ya watahiniwa ambao hawakufanya mtihani ili waweze kubaini sababu ya kutofanya mitihani hiyo.

Kadhalika, alitangaza operesheni itakayofanyika wilaya nzima kubaini wazazi na walezi wanaojihusisha na vitendo hivyo ili wachukuliwe sheria stahiki.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Misungwi, Abdi Makange alisema kuwa jamii ya wasukuma imekuwa na dhana mbovu ya kuamini juu ya kuozesha watoto wadogo na kuwaachisha masomo, hivyo kuahidi kutowavumilia na kuwachukulia hatua kali za sheria pindi watakapogundulika.

# Ujenzi Daraja la Kitengule wafikia asilimia 99.9

**Na Shaban Njia,** KAGERA

UJENZI wa Daraja la Kitengule (mita 140) linalounganisha Wilaya ya Missenyi na Karagwe mkoani Kagera limekamilika kwa asilimia 99.9.

Daraja hilo lililogharimu zaidi ya Sh.bilioni 31.5 limetekelezwa na Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) kwa kushirikiana na kiwanda cha sukari cha Kagera Sugar lengo likiwa ni kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa bidhaa zikiwemo miwa inayotolewa upande wa Karagwe kwenda kiwandani.

Akielezea utekelezaji wa mradi huo muhimu mkoani hapa, Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Kagera, mhandisi Ntuli Mwaikokesya alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Septemba, 2022 ukigharimu Sh. bilioni 31.55.

Alisema kuwa kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 26.5 zilitolewa na serikali sawa na asilimia 84, huku Sh. bilioni tano zikitolewa na kiwanda cha Kagera Sugar sawa na asilimia 16, ukamilishwaji wa daraja hilo ukitajwa kuondoa adha ya usafirishaji mali ghafi kutoka umbali wa zaidi ya kilometa 28. Mwaikokesya alisema, mwaka jana Rais Dk. Samia Suluhu Hassani alitembelea mradi huo na kushauri ujenzi usiishie kwenye daraja pekee na badala yake waendelee na ujenzi wa barabara ya kilometa 25 inayopita ndani ya kiwanda mpaka Bunazi.

Ofisa Kilimo kutoka katika kiwanda cha Kagera Sugar, Filibert Fideli alisema daraja hilo limepunguza mzunguko wa kuwafikia wakulima wao na kuwapatia elimu ya kulima miwa kisasa tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Aidha, alimshauri mkandarasi kukamilisha ujenzi wake kwa kuweka alama za usalama barabarani ili kukabiliana na ajali ambazo zinaweza kujitokeza kwani magari ya kiwandani, abiria na mizigo yanapita kwa kasi hali ambayo inawatia hofu.

Hivyo, aliahidi kulinda miundombinu ili iendelee kuwanufaisha na kukuza uchumi wa nchi.



Ukurasa 12

**‘Vikumbo’ vigogo hawa Afrika, vilivyoacha maswali bila majibu**




Ukurasa 13

Hakuna tija kuchafuana kwa jambo linaloibeba nchi


# siasa

JUMATANO NOVEMBA 15, 2023

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

**Mwanamke ‘mjeshi’ harakati za ukombozi wa mwanamama**

MISWADA BUNGENI

# Yajayo hayafurahishi CUF yaona walakini, imekula kwao

• Hawaridhiki wakurugenzi kubaki, m/kiti, makamu na mkurugenzi kuwa wateule

**Na Sabato Kasika**

HADI ya kupeleka miswada ya kurekebisha sheria zinazohusu uchaguzi, ili kupunguza malalamiko ya kukosekana haki katika chaguzi, imetimia. Ni baada ya miswada hiyo kutinga bungeni wiki iliyopita.

Miswada hiyo ni pamoja na ule wa sheria ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani ya mwaka 2023, wa sheria ya tume ya uchaguzi ya 2023 na mwingine ukihusu marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 2023.

Novemba 10 sheria hizo zilitinga bungeni ili kufanyika marekebisho, ikiwa ni sehemu ya mchakato wa kufanikisha kile ambacho wadau wamekuwa wakikitamani kuona Tanzania inakuwa na uchaguzi huru, wa haki na unaokubalika.

Baadhi ya wadau wanazungumza na Nipashe kuhusu uamuzi huo wa serikali kuanza kuyafanyia kazi matakwa ya wanasiasa na wanaharakati wa mabadiliko ya kidemokrasia, wanaotaka tume huru ya uchaguzi na uchaguzi usiolalamikiwa.

Bob Wangwe ni Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), anayesema kinachoendelea sasa kinaonyesha hakuna utashi kisiasa, kutokana na serikali kurudisha wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi, jambo ambalo linalalamikiwa.

“Wakurugenzi walikataliwa ndani na nje za mahakama za Tanzania na ile ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, lakini serikali imewarejesha tena kusimamia uchaguzi. Hapa hakuna utashi wa kisiasa,” anasisitiza.

Anaongeza kuwa wajumbe wa tume, viongozi, watu wengine wanaoweza kumsaidia mkurugenzi wa uchaguzi sifa zao zimeainishwa kwamba wasiwe wamejiunga na chama chochote cha siasa.



Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya. **PICHA: MTANDAO**

“Tunaona kama tume haiko huru, kitendo hicho kitaendelea kuathiri uhuru wa tume, lakini labda wakati huu wa mijadala, kabla ya miswada kuwa sheria tusuburi watunga sheria wasikilize maoni ya wananchi ili tuweze kupata sheria ambazo zitaonyesha kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, ana nia ya dhati ya kurekebisha mifumo yetu ya uchaguzi,” anasema.

Aidha, anaongeza kuwa kuna vifungu vingine vya sheria ya uchaguzi haviwezi kubadilishwa, kwa ajili kusaidia uhuru wa tume kama katiba haijabadilishwa.

“Kwa hiyo vipengele ambavyo vinahusiana na uhuru wa tume, kwa mfano kupinga matokeo ya urais, kuwapo mgombea huru ni lazima kupelekwa mapendekezo madogo bungeni, kwa ajili ya kufanya marekebisho madogo ili tume iwe huru,” anasema.

**HAKUNA DHULUMA**

Kada wa CCM, Abdulkarim Atiki, anasema uamuzi wa kupeleka miswada hiyo bungeni, ni wazi kwamba Rais Samia hataki dhuluma. Siku ya kiama hataki kwenda kuulizwa kwa Mola wake kama amehusika katika dhuluma hasa kwenye uchaguzi, anataka haki itendeke wananchi wapate wawakilishi ambao wamewachagua wenyewe badala ya kupata ushindi wa mezani.

“Tume ya uchaguzi imekuwa ikilaumiwa sana, maana yake ni kwamba kuna jambo haliko sawa, hivyo, kupelekwa kwa muswada wa sheria ya tume ya uchaguzi wa mwaka 2023, ina maana Rais anataka tume huru isiyo na makandokando, Watanzania waridhike nayo,” anasema Atiki.

Kadhalika, nchi ikiwa na tume huru, hata mabadiliko ya katiba yatakuja yenyewe kupitia kwa wawakilishi wa wananchi ambao wamechaguliwa kihalali, na kwamba watawakilisha mawazo ya wananchi.

“Lakini baadhi ya wawakilishi wamekuwa wakipata ushindi wa mezani wa kupita bila kupingwa badala ya kushindana kwa hoja majukwaani, matokeo yake wananchi wanakosa wawakilishi halali wa kusimamia maslahi yao, hilo mama amelikataa,” anasema.

Mwanasiasa huyo anasema kupelekwa bungeni kwa miswada hiyo mitatu, ni dalili tosha kuwa Rais Samia si kiongozi anayekumbatia dhuluma, na kuongeza kuwa anataka kila mmoja apate haki yake kwa kuzingatia kwamba Tanzania inajengwa na Watanzania wote bila kujali vyama wanavyotoka.

**IMEKULA KWAO**

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, Magdalena Sakaya, anasema miswada hiyo kupelekwa bungeni, kuna hatua imefanyika na kwamba kama taifa limesogea kwenda mbele.

Hata hivyo, anafafanua kuwa imekula kwao, kwa kuwa walitaka kuwapo tume huru ya uchaguzi, na kwamba mwenyekiti na makamu waombe nafasi hizo kulingana na sifa zao.

“Zamani, tume ya uchaguzi kuanzia mwenyekiti, mkurugenzi na wajumbe, walikuwa wanateuliwa na Rais, na sisi tunataka wote wasiteuliwe bali wapatikane kulingana na sifa zao,” anasema Magdalena.

**INAENDELEA UK. 12**

# ‘Vikumbo’ vigogo hawa Afrika, vilivyoacha maswali bila majibu






Rais wa Ujerumani Frank-Walter Steinmeier na Mfalme Charles 111 wa Uingereza. Wawili hao walizuru Afrika Mashariki hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

VIONGOZI wakuu kutoka Ulaya, Mfalme Charles III wa Uingereza pamoja na Rais wa Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier, waliwasili wakati mmoja kwa ziara za kikazi kwenye nchi mbili za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Wanazitembelea Kenya na Tanzania na baada ya kutua walipokelewa na Marais William Ruto wa Kenya akimkaribisha Mfalme Charles III na Rais Samia Suluhu Hassan, alimkaribisha Steinmeier.

Mbali na ajenda tofauti ikiwamo za kimahusiano, nyingine kuu zilizotawala vyombo vya habari vya ndani na kimataifa, ilikuwa ni kuomba radhi kwa nchi za EAC.

Kwanza huko Kenya, Mfalme Charles III, alikiri uovu wa Uingereza dhidi ya Wakenya kutokana na athari za vita ya Mau Mau vilivyoanza mwaka 1952 hadi 1960 hasa vifo lakini hakuomba msamaha moja kwa moja, akisema hawezi kubadilisha historia.

Na katika ziara hiyo ya siku nne, Mfalme Charles III aliyeambatana na mkewe Malkia Camilla, alitakiwa aseme neno la kuomba radhi, lakini alikwepa.

> Nataka kuwahakikishia kuwa sisi Wajerumani, tutashirikiana nanyi kwa pamoja kutafuta majibu ya maswali ambayo hayajajibiwa ambayo hayawapi amani.

Kadhalika, Rais wa Ujerumani, Steinmeier, aliyekuwa nchini siku tatu alifika Songea mkoani Ruvuma, kuangalia kumbukumbu ya vita vya Majimaji na kutembelea Shule ya Msingi Majimaji. Ndipo alipowaomba radhi Watanzania kutokana na athari za vita hasa vifo.

Kwake, Mfalme Charles III kuzuru Kenya, ni mara ya kwanza, tangu alipochukua madaraka baada ya mama yake, Malkia Elizabeth II, kufariki Septemba, mwaka jana.

### VIFO EAC

Kwa mujibu wa vyombo vya habari kimataifa, Sauti ya Amerika (VOA), RFI pamoja na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), zaidi ya watu 10,000 waliuawa na wengine kuteswa wakati wa ukandamizaji wa kikatili wa uasi wa Mau Mau katika miaka ya 1950.

Vinaeleza, mojawapo ya uasi wa umwagaji damu zaidi ulisababishwa na Dola ya Uingereza na mwaka 2013 Uingereza ilijutia tukio hilo, na kulipa paundi ya Uingereza milioni 20 (sawa na dola za Kimarekani milioni 24) kwa zaidi ya watu 5,000 ingawa wengine walihisi haikutosha.

Wakati wa mamlaka ya kikoloni, ilitangazwa hali ya dharura ili kukabiliana na kampeni ya msituni ya Mau Mau dhidi ya walowezi kutoka Ulaya.

Mfalme huyo wa Uingereza, alilitembelea jiji la Nairobi pamoja na mji wa Bandari wa Mombasa, lakini siyo Nanyuki, ambako kuna kituo cha mafunzo ya Jeshi la Uingereza Kenya (BATUK).

### VITA MAJIMAJI

Kadhalika, kwenye vita ya Majimaji huko Songea, vilivyoanza 1905 hadi 1907, Rais Steinmeier, aliyetembelea Tanzania, kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba mosi, mwaka huu, anafikisha ajenda ya msamaha.

Anaeleza kufedheheshwa kwake na uhalifu uliofanywa wakati wa utawala wa kikoloni wa Ujerumani, wakati huo Tanganyika ikiwa chini ya ukoloni wake. Rais huyo anaahidi kuongeza uelewa kuhusu madhila hayo katika nchi yake, kwa mujibu wa tovuti ya Idhaa ya Ujerumani (DW).

Kadhalika taarifa hizo za Ujerumani kuomba radhi, zilichapishwa na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania katika ukurasa wake wa mtandao wa X, zamani Tweeter, ikisema:

“Ningependa kuomba radhi kwa kile ambacho Wajerumani walikifanya kwa mababu zenu hapa,” anasema Rais Steinmeier alipotembelea Makumbusho ya Vita vya Maji Maji, yaliyopo mji wa Songea, mkoani Ruvuma, Kusini mwa Tanzania.

Tanganyika ambayo baadaye iliungana na Zanzibar na kunda Tanzania, ilikuwa sehemu ya Afrika Mashariki ya Ujerumani (German East Africa), iliyojumuisha pia Rwanda na Burundi, ilishuhudia umwagaji damu mkubwa zaidi katika historia ya ukoloni huo kati ya mwaka 1905 na 1907.

Wataalamu wanasema kati ya watu 200,000 na 300,000 kutoka jamii za makabila ya asili waliuawa kikatili na uharibifu wa mashamba na vijiji ulifanywa na wanajeshi wa Ujerumani, wakati wa kile kinachoitwa ‘Uasi wa Maji Maji.’ Akieleza kufedheheshwa kwake kwa tukio hilo, Rais Steinmeier amesema, Ujerumani iko tayari kufanya kazi na Tanzania kuyatathmini kwa pamoja yale yaliyopita.

“Kilichotokea hapa ni historia inayotuhusu sisi na ninyi ni historia ya mababu zetu, mababu zenu na babu zetu wa Ujerumani,” akasema, huku akiahidi “nitazichukua simulizi hizi pamoja nami hadi Ujerumani, ili watu wengi zaidi katika nchi yangu wazijue.”

“Nataka kuwahakikishia kuwa sisi Wajerumani, tutashirikiana nanyi kwa pamoja kutafuta majibu ya maswali ambayo hayajajibiwa ambayo hayawapi amani,” anaongeza.

Licha ya kuondoka Uingereza Charles ameacha maswali mengi akipingwa kuwa licha ya kueleza kuguswa na uovu uliotokea hakutamka kwa niaba ya serikali yake kuwa anawaomba msamaha Wakenya kwa uhalifu huo.

Hata hivyo Steinmeier pengine familia ya Chifu Songea Mbano, ilitegemea angetangaza kurudishwa kichwa chake mara moja lakini hilo nalo ni jambo la kuendelea kusubiri.

# Yajayo hayafurahishi CUF yaona walakini, imekula kwao

**INATOKA UK. 11**

Anaongeza kuwa kinachokwenda kufanyika ni kwa wajumbepekee kupata nafasi kulingana na sifa zao , lakini mwenyekiti, makamu na mkurugenzi wataendelea kuteuliwa na Rais.

“Kuna suala pia la mgombea huru, kura za rais kuhojiwa mahakamani, hayo yote yamewekwa pembeni, ndiyo maana ninasema imekula kwetu, kwani tumeambulia la mgombea kupita bila kupingwa tu,” anasema.

Magdalena anafafanua kuwa pamoja na kwamba uamuzi wa kupelekwa miswada hiyo bungeni kuna hatua ambayo imefanyika bado safari ni ndefu ya kufikia demokrasia ya kweli.

### UCHAMBUZI KWANZA

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu, anasema chama hicho kimeielekeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Chama kuichambua miswada hiyo iliyosomwa kwa mara ya kwanza bungeni.

“Ni jambo la faraja kuwa hatimaye miswada hii imewasilishwa bungeni. Yapo masuala yaliyotufurahisha kama vile kuondosha suala la kupita bila kupingwa. Lakini, yapo masuala yanayohitaji maboresho,” anasema Ado.

Anasema wanatamani uchaguzi ujao uwe, haki na kuaminika, na kwamba chama chao kitafanya uchambuzi wa kina wa miswada yote mitatu kisha utawasilishwa kwenye vikao vya chama kabla ya kuwasilishwa bungeni.

“Tunapenda pia kurudia rai yetu kuwa itakuwa ni jambo la ajabu kwamba tume ya uchaguzi itakayoundwa isisimamie uchaguzi wa serikali za mitaa. ACT Wazalendo hatuungi mkono uchaguzi huo kusimamiwa na TAMISEMI,” anasema.

Anafafanua kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa ACT Wazalendo inaongozwa na Wakili Omar Said Shaaban, ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK) akisaidiwa na jopo la mawakili kadhaa wa chama.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson. **PICHA: MTANDAO**

# Hakuna tija kuchafuana kwa jambo linaloibeba nchi

**Na Reubeni Lumbagala,** KONGWA

TANZANIA si kisiwa, ujenzi wake unahusisha mengi ikiwa ni pamoja na kujenga mahusiano bora kati yake na mataifa mengine, kusaini mikataba na protokali mbalimbali pamoja na kuridhia.

Ni katika muktadha huo, Tanzania imekuwa mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa kuanzia Mtangamano wa Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Afrika (AU) kwani yapo manufaa mengi kujenga mahusiano bora baina ya nchi hii na jumuiya hizo.

Ujenzi wa nchi na kuifanya uhusiane vyema na mataifa mbalimbali dunia si kazi ya viongozi peke yao bali ni jukumu la raia pia, wawe viongozi pamoja na wananchi wote katika ngazi mbalimbali mijini na vijijini.

Hivi karibuni Tanzania imeongeza ushiriki wake katika kuyaongeza mabunge dunini , ni baada ya Mtanzania kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Dunaini (IPU).

Ni fursa nyingine kwa nchi kujitangaza kimataifa na kuonyesha weledi wake kwenye nyanja mbalimbali za ushirikiano.

Katika uchaguzi huo unaoitambulisha Tanzania kimataifa zaidi, Spika Dk. Tulia Ackson, ndiye aliyepeperusha bendera ya ushindi akishinda kwa kishindo kwa kupata kura nyingi.

Hata hivyo, mambo hayakuwa rahisi, na ugumu wa kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia kwa Dk. Tulia ukianzishwa na Wtanzania wenyewe.

Kumbe wapo baadhi Watanzania walioamua kumchafua Spika ili asichaguliwe kushika nafasi hiyo ambayo ni muhimu kufanikisha azma ya serikali kuifungua nchi kimataifa.

Ukweli huo unawekwa hadharani Oktoba 30, 2023, katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma kwenye hafla ya kumpongeza Dk. Tulia kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa IPU na pia kuingia kwenye rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo.

Akizungumza katika hafla hiyo, anaeleza namna alivyokutana na magumu wakati wa uchaguzi huo huku baadhi ya Watanzania wakiwa kinyume naye.

"Uchaguzi ule ulikuwa mgumu sana na hii ni kutokana na mitandao ya kijamii kutumika kunichafua. Tena waliofanya hivyo ni Watanzania wenzetu ambao walikuwa wakiungana na wengine kunikwamisha nisishinde nafasi hii," anasema Dk. Tulia.

Kiukweli pengine si jambo jema kuona fursa adhimu nchi iliyoipata inapigwa teke kwa kumchafua mgombea ambaye ushindi wake unatangaza taifa katika uga wa juu diplomasia za kimataifa.

Ushindi wake pia ni darasa muhimu katika kuhamasisha wasichana na wanawake kujiamini katika nyanja zote mbali na kuzidi kuitangaza nchi kimataifa na kuonyesha uwezo mkubwa kinamama walio nao.

Kasumba hiyo mbaya ya kuchafuana si jambo jema hasa linapokuja suala la kitaifa lenye maslahi kwa nchi linalosababisha wengine kujiuliza, hivi kumchafua Mtanzania mwenzako katika kinyang'anyiro kama hicho inatokana na wivu, husuda, uadui au ujinga? Nimejiuliza sana.

Kuungana na adui dhidi ya ndugu yako ni kukosa uzalendo.

Ni katika muktadha huo, Dk. Tulia anaendelea kusema: "Ni jambo la ajabu sana Watanzania kuungana na adui zao kulipiga vita taifa lao. Niwaombe linapotokea suala la kitaifa tuwe kitu kimoja badala ya kuungana na adui zetu kuumizana wenyewe kwa wenyewe."

Anasema nchi nyingi zilisema hazitaweka wagombea ili kuipa nafasi Tanzania kuchukua kiti cha urais cha umoja wa mabunge lakini maneno ya kwenye mitandao yakawapa nguvu ya kuleta wagombea! "Lakini kwa kuwa Mungu alikuwa amepanga Tanzania ishinde hakuna kilichobadili hilo," anasema.

Kasumba hiyo imo pia katika sekta ya michezo, inapokuja timu kutoka nje ya nchi kucheza na timu za ndani hususan zile zinazofahamika kiukubwa, baadhi ya mashabiki wa Tanzania hushangilia wageni na kuachana na 'mtoto wa nyumbani'.

Wanafanya hivyo huku wakijua au kutojua kwamba matokeo yoyote mazuri ni faida kwa nchi mbali na klabu husika.

Kwa mfano, matokeo mazuri ya timu katika mechi za kimataifa yamesababisha timu nyingi kushiriki mashindano ya African Footbal League na hata kama baadhi ya timu zimetolewa lakini jina la Tanzania limetajwa na wachezaji kupata uzoefu.

Ushindi katika mechi za kimataifa, unaongeza kujiamini na hata kuwafanya wapinzani wawaogope pia tofauti na zamani walipokuwa wanadharau sana na wanapocheza na Tanzania walikuwa na kiburi cha ushindi nje na ndani ya uwanja.

Bila shaka, kushabikia timu hizo kubwa si uadui na hivyo wanaweza kuombeana mabaya na kukinzana wanapocheza ligi ya ndani lakini zinapokutana na timu za nje, ni vyema kuoneshe uzalend na pale unaposhindwa kaa kimya na si kumshangilia au kumrahisishia mgeni ili amshinde mwenyeji.

Tanzania ndiyo nyumba yetu, ni vyema viongozi na wananchi kwa pamoja kuijenge ipendeze kwenye macho ya wageni hata kama kwa ndani kuna misuguano.

Mathalani, mashindano mapya ya African Football League (AFL) yalipofunguliwa Tanzania ilikuwa mwenyeji na kuvuta dunia kuja au kuiangalia mashindano yakianzia Dar es Salaam, ikumbukwe kufanikiwa kwa ujenzi wa nyumba hii kutategemea sana umoja na upendo baina ya Watanzania.

Kumbukeni hatupaswi kugombania fito wakati tunajenga nyumba moja, kusimama kwa nyumba yetu ni sifa yetu sote na kubomoka na kuonekana chafu mbele ya macho ya wageni ni fedheha kwa wote.

Kama wahenga wasemavyo "umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu" ndivyo ushirikiano wa pamoja wa viongozi na wananchi ulivyo nguzo muhimu ya kufanikisha ujenzi wa Tanzania na kuipatia maendeleo endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Ni dhahiri kuwa na sauti moja na nia moja ili taifa lifanikiwe katika harakati na jitihada za kuletea maendeleo ndani ya familia ya Tanzania na katika uchumi mpana na uwanja wa kiushirikiano.

Kwa mtazamo huo, hapo awali ` hususan kipindi baa la UVIKO - 19 taifa liliisumbua dunia, uhusiano wa Tanzania na baadhi ya mataifa mengine ulilegalega kiasi, pengine kutokana na misimamo yake huku wengine wakishindwa kuielewa hasa pale ilipoleta ubishani wa matumizi ya chanjo.

> Rais au wengine wanavyomwita mwanadiplomasia namba moja, amekuwa akihimiza kujenga mahusiano mazuri na mataifa mengine kwa ajili ya manufaa ya pamoja na mafungamano zaidi.

Hata hivyo awamu ya sita Dk. Samia Suluhu Hassan, imekuwa na vipaumbele kadhaa katika kufanikisha maendeleo ya nchi na uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine kwenye nyanja mbalimbali za kiuchumi na ushirikiano kidiplomasia.

Moja ya kipaumbele cha Rais Samia ni kuifungua nchi kimataifa na kuhimiza diplomasia ya uchumi inayoelekeza kualika wawekezaji na kujenga uwanja mpana wa kiuchumi unaoshirikisha Watanzania na wageni kutoka mataifa mbalimbali.

Rais au wengine wanavyomwita mwanadiplomasia namba moja, amekuwa akihimiza n kujenga mahusiano mazuri na mataifa mengine kwa ajili ya manufaa ya pamoja na mafungamano zaidi.

Mabalozi wanaoiwakilisha nchi katika mataifa mbalimbali wamekuwa wakihimizwa kufanya kazi kwa bidii hasa katika kutafuta fursa ambazo zitalinufaisha taifa ili kuchagiza gurudumu la maendeleo. Aidha, wanahimizwa kuvutia wawekezaji kuja Tanzania kwa wingi ili kuwekeza na hivyo kutengeneza ajira, kukuza uchumi, kuongeza mapato na kasi ya maendeleo.

Kimsingi, juhudi kubwa zinafanyika kuifungua nchi kimataifa kwani kufanikiwa kwa hili, kuna uhusiano wa moja kwa moja na kufanikisha mipango ya kimaendeleo kwa ustawi wa Tanzania na raia wake.

***Maoni: 0620 800 462.***

## JUKWAA LA VIONGOZI

MARY RUSIMBI

# Mwanamke 'mjeshi' harakati za ukombozi wa mwanamama

• Anaanzia TGNP sasa mfuko wa ruzuku,aahidi yajayo ni furaha

**Na Mwandishi Wetu**

MWANZONI mwa 1990, wanawake Tanzania walipata nguvu mpya na kuanza harakati za mapambano ya kujikomboa na ukandamizaji kama mfumo dume, umaskini, elimuduni , kukosa uwakilishi wa kisiasa na uongozi wa kuteuliwa.

Ni harakati ambazo zilihitaji wanawake wanajeshi wa kuleta ukombozi ili kukabiliana na mifumo kandamizi ya muda mrefu, kudai haki kwa nguvu na kuleta pambazuko jipya kwa kinamama na watoto wa kike.

Kundi hili lilinyanyaswa na mila kandamizi, ukatili ndani ya familia na jamii nzima, kwa kuwa usawa wa kijinsia haukuwa kipaumbele.

Jukwaa la Uongozi leo, linamtazama mwanajeshi wa ukombozi wa mwanamke wa Tanzania, Mary Rusimbi, ambaye anaandika historia katika kudai haki na usawa kwa mama na binti wa taifa hili.

Mary kwa kushirikiana na wanaharakati kadhaa akiwamo Profesa Marjorie Mbilinyi, Gema Akilimali, Fides Chale, Dk. Demere Kitunga na wengine kadhaa mwaka 1993 wanaanzisha Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Ni shirika la kiraia la wanaharakati wanawake lenye lengo la kuleta vuguvugu la mageuzi la ufeminia (feminism) na kuhamasisha Tanzania yenye usawa wa kijinsia katika kuandaa, kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo inayomgusa kila mmoja. TGNP wiki iliyopita imetimiza miaka 30.

Imefanya mengi mfano, imekuwa sauti ya wanawake, kutetea haki zao na kutaka usawa wa kijinsia huku ikiamsha harakati zilizofanikisha ushindi kwa wanawake kwenye vikwazo vingi.

Mfano, Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA), inayotoa adhabu makosa ya ubakaji, ukeketaji na unyanyasaji watoto kingono ni zao la wafeminia TGNP.

Kadhalika, Sheria ya Ardhi, iliyorekebishwa na kutamka wazi kuwa kama ilivyo kwa wanaume wanawake wana haki ya kumiliki na kutumia ardhi kwa maendeleo yao, shirika limehusika sana.

Aidha, kufanya uchambuzi wa bajeti na kutoa mapendekezo ya sera za kijinsia, lakini pia kufanikisha kuanzishwa kwa vituo vya taarifa na maarifa na mabunge ya wananchi kuiwezesha jamii kupaaza sauti ni tunda lake.

Vyote, vimewajengea uwezo wanawake na wananchi kutumia majukwaa vijijini au popote kuchambua hali zao, kuibua changamoto na kuziwasilisha serikalini, zifanyiwe kazi kuboresha maisha yao. Baada ya hamasa na kuamsha harakati za ufeminia ambalo ni vuguvugu la wanawake kwenye harakati za kujikomboa, ni wazi uamsho umekuja na asasi za kiraia ambazo zinahitaji fedha na ruzuku ili kujiendesha.

Pamoja na kumjengea mwanamke uwezo atafanikishaje harakati za kujikomboa? Ni suala linawapasua kichwa Mary Rusimbi na wanaharakati wengine, kupata majibu, ni kwa vipi taasisi zinazofanyakazi na jamii zitapata fedha zitaendesha harakati?




Janeth Mawinza Mkurugenzi wa Shirika la WAJIKI, pamoja na wadau wa bodaboda, wanaopambana rushwa ya ngono kwa wanafunzi, kwa uhisani wa WFT-T.

> Utetezi wa haki za mwanamke kwenye ajira za ndani, unawafungua wafanyakazi hao kujua umuhimu wa kuingia mikataba ya maandishi baina yao, waajiri na serikali inayowakilishwa na wajumbe wa serikali za mitaa.



Mary Rusimbi mwanaharakati wa ukombozi wa mwanamke kimapinduzi. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Ndiyo ujio wa Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Women Fund Tanzania Trust (WFT-T) wanaofanya harakati za kumkomboa mwanamke kimapinduzi.

Mwaka 2008 Mary anashirikiana na wanaharakati kuanzisha WFT-T shirika la kwanza na la kipekee linalotoa ruzuku kuendeleza shughuli za utetezi wa haki za wanawake hasa walio ngazi za jamii.

Lengo kuu ni kuchagia harakati za kutetea haki za wanawake na kuendelea kuwawezesha pamoja na mikakati ya ujenzi wa vuguvugu la utetezi wa pamoja ili kukuza haki na usawa wa wanawake kimapinduzi .

Ruzuku hulenga shughuli zinazopeleka harakati za wanawake katika ngazi za chini na nyingine inalenga ujenzi wa muungano wa mashirika na mitandao ya wanawake katika ngazi ya taifa ili kuleta mageuzi ya kuwakomboa wanawake na watoto wa kike kutoka minyororo ya ukandamizwaji.

WFT-T, ina mengi ya kujivunia kama kutoa ruzuku ndogo na za kati kwa mashirika ya watetezi wa haki za wanawake ngazi ya kitaifa na kijamii ili kuimarisha na kuendeleza mikakati ya ujenzi wa nguvu za pamoja.

Kwa kuwapa ruzuku pamoja na kuwajengea uwezo wanawake wa ngazi mbalimbali, limefanikisha harakati likiwa na mitandao kwenye mikoa kadhaa mfano Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Pwani. Mtandao wa Kupambana na Rushwa ya Ngono uko Dar, unaoelimisha wanafunzi shuleni kuifahamu na kuikataa rushwa ya ngono.

Aidha, mfuko kupitia kampeni ya 'vunja ukimya usafiri bila rushwa ya ngono unawezekana', umewafikia madereva mbalimbali wa mabasi ya mikoani, daladala, bodaboda na bajaji.

Maderava hao kwa mazoea hutumia vyombo vyao kuwadhalilisha wanafunzi na kusababisha mimba za utotoni, utoro, ubakaji na ngono kinyume cha maumbile

Ni kampeni, inayotoa ujumbe kupitia stika , vizibao (reflectors), mabango na fulana vyenye ujumbe wa kukataa na kukomesha rushwa ya ngono. Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo, WAJIKI ni mshiriki mkuu.

Mkoani Mwanza mamia ya wanawake wanaumizwa na ukatili na unyanyasaji kwenye visiwa wilayani Ukerewe vikijumuisha Ukara, Ukerewe na Nansio.

Unyanyasaji visiwani unachangiwa na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha upungufu mkubwa wa samaki na dagaa visiwani, nishati kwa ajili ya kupikia na kazi ili kujikimu.

Katika hali hiyo wanawake wanalazimika kuomba kazi kwenye kambi za uvuvi ambako wanaombwa rushwa ngono ili kupewa kazi, aidha watoto wanatumikishwa bila ujira kwenye kambi za uvuvi ili kukusanya na kuchambua dagaa na wengine wakifanyiwa ukatili kingono.

Mfuko wa WFT-T umewafikia ukishirikiana na asasi za kiraia kama Sauti ya Wanawake Ukerewe kutoa somo kuachana na unyanyasaji, ukatili kwa wanawake na kuwafundisha mbinu mbadala kukabili mabadiliko ya tabianchi,

Aidha, ruzuku ya WFT-T imewafikia watetezi wa haki za watumishi wa nyumbani ambao wengi ni wanawake, tena baadhi ni watoto wakinyonywa kwenye ajira ya watoto.

Mfuko unaufadhili Mtandao wa Wafanyakazi wa Nyumbani katika mikoa kadhaa mfano Mwanza, Morogoro na Pwani na kuibua changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi.

Yanayoibuliwa ni pamoja kutojua kiwango cha mshahara au ujira wao, kwa mujibu wa sheria, takwimu za WFT-T zikionyesha kuwa watumishi hao wamefahamishwa viwango vya kima cha chini cha mshahara kwa mujibu wa tangazo la serikali No: 687/2022.

Aidha, mfuko huo umefanikisha kupata taarifa za sensa ya wafanyakazi hao ukieleza kuwa wapo 250,000 wanaofanyakazi kwa wanadiplomasia na wafanyabiashara wakubwa, wakati wanaofanyakazi kwa maofisa wenye stahiki ni 200,000 na wengine 120, 000 wanafanyakazi na kuishi na waajiri wao sehemu mbalimbali.

Mchakato wa kufikia watumishi au kundi hilo lenye idadi kubwa ya wanawake ambao wananyanyaswa kijinsia, kutumikishwa bila ujira wala mikataba ya maandishi ni jambo ambalo Mary na wana harakati waliliona na kulipatia ufumbuzi.

Utetezi wa haki za mwanamke kwenye ajira za ndani, unawafungua wafanyakazi hao kujua umuhimu wa kuingia mikataba ya maandishi baina yao, waajiri na serikali inayowakilishwa na wajumbe wa serikali za mitaa.

Kwa ujumla ujumbe wa Mary Rusimbi kwa wanaharakati wa kifeminia,unabaki kuwa 'ndiyo kwanza mapambano yanaanza.'





## Kamati ya Bajeti yaridhishwa utekelezaji miradi Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeridhishwa na mwenendo wa utekelezaji wa miradi inayotekelezwa ndani ya Mkoa wa Dodoma ikiwemo mradi wa Bwawa la Membe na Skimu ya Umwagiliaji Chinangali chini ya Mradi wa Building Better Tomorrow (BBT) wilayani Chamwino.

Akizungumza juzi jijini hapa, Mwenyekiti wa Kamati hiyo na Mbunge wa Kilindi mkoani Tanga, Omary Kigua alisema ziara hiyo ina lengo la kutembelea na kukagua maendeleo ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo.

"Tumeridhika na shughuli zinazoendelea hapa na kiasi cha fedha ambacho kimetumika hakika kinasadifu kwamba kazi mnaisimamia vizuri" alisema Kigua.

Aidha, aliwahimiza wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali akisema kukamilika kwa mradi huo itakuwa chachu kwa wananchi wote ambao wapo jirani na maeneo hayo ya miradi.

"Kwa kuwa wao ndiyo wanufaikaji wa kwanza na ndiyo dhamira ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambayo ni kuinua maisha ya wananchi wa chini" alisema.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde alitumia fursa hiyo kuelezea azma ya serikali katika kuhakikisha wanamuwezesha mkulima kuzalisha kipindi chote cha mwaka bila kutegemea mvua.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alimshukuru Rais Samia kwa kufanya mapinduzi ya kilimo ndani ya mkoa ambayo yatasaidia kuondoa njaa, udumavu na kitakuwa chanzo cha uchumi kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

# Wafugaji wadaiwa kumshambulia, kumjeruhi ofisa afya Mpwapwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISA afya wa Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Ismail Wabu, amenusurika kifo baada ya kuvamiwa na kupigwa na watu wanaodaiwa kuwa ni jamii ya wafugaji wakati akitekeleza majukumu yake ya kuhamasisha matumizi ya vyoo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma alipolazwa ofisa huyo alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11 alfajiri wakati wakizunguka kwenye makazi ya watu na kutoa elimu ya matumizi bora ya vyoo.

"Tulikuwa tukitoa elimu ya usafi wa mazingira na matumizi bora ya vyoo kwa wakazi wa eneo la Kikiji cha Igoji One eneo ambalo ni la jamii za wafugaji ambao wamekuwa hawatumii vyoo.

"Tulienda nyumba ya kwanza tukamkuta mama mmoja tukamchukua, tukaenda ya pili tukamkuta kijana mmoja tukamchukua na tukaenda nyumba ya tatu hatukukuta watu mara tukasikia mawe yakaanza kurushwa na wengine kupiga miluzi ndipo likatokea kundi la watu wengi wakaanza kutukimbiza" alisema.

Alisema baada ya kundi hilo kutokea walianza kukimbia na yeye kujikwaa na kuanguka ndipo walipomvamia na kuanza kumpiga kwa fimbo hadi kupoteza fahamu.

"Nilipoanguka nikawaomba msamaha wasinipige nikiwaambia kuwa sisi hatuna nia mbaya kwani tunachotaka ni kutoa elimu ya usafi wa mazingira na ujenzi wa vyoo hawakunielewa na wengine walikuwa wakisema niuawe, mmoja akanipiga fimbo ya kichwa ndipo nilipopoteza fahamu" alisema.

Alisema alipozinduka alijikuta katika vichaka huku watu wakiwa wamemzunguka ambao walimsadia kumtafutia usafiri wa pikipiki na kupelekwa katika Kituo cha Afya cha Mima.

"Nilipelekwa katika kituo hicho cha afya na kupatiwa matibabu lakini walinihamishia kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa na baadaye ikahitajika nifanyiwe kipimo cha CT scan ndipo wakanipatia rufani ya kuja hapa" alisema.

Alisema baada ya kufanyiwa kipimo hicho imebainika kuwa taya zake zote zimevunjika, hivyo anasubiri kupatiwa matibabu kulingana shida yake.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Dk. Rahim Hangai, alithibitisha kumpokea majeruhi huyo.

Alisema: "Kama ambavyo mmemuona walimpiga sana na amenusurika kifo kwani walikuwa wamuuwe ni Mungu tuu lakini hawa watu inasemekana siyo mara ya kwanza kufanya tukio kama hili nasikia hata kipindi cha nyuma walishampiga mtumishi wa halmshauri.

"Hawa ni jamii ya wafugaji ambao wao hawataki kujenga vyoo hivyo wakaamua kuwapiga wataalam wetu ambapo huyu mmoja alianguka wakati akikimbia na kumvunja taya zake na hivi sasa amelazwa katika hospitali ya rufaani ya mkoa wa Dodoma"alisema.



Baadhi ya wananchi wakiangalia magari yaliyopata ajali baada ya kugongana katika eneo la Kisasa, jijini Dodoma jana. Hakuna mtu aliyejeruhiwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kamati ya Bunge yaagiza TRA, TANROADS kushirikiana

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeitaka serikali kuzisimamia taasisi zake ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ili ziwe zinafanya kazi kwa kushirikiana.

Imesema taasisi hizo zimekuwa kikwazo cha kukwamisha baadhi ya miradi ikiwamo ya umeme na kusababisha ongezeko kubwa la gharama za miradi inayotekelezwa nchini.

Wabunge wa kamati hiyo walitoa agizo hilo jana kwa serikali baada ya kutembelea mradi wa usafirishaji umeme uitwao Backborn Transmission Investment Project (BTIP) ambao unalenga kuziunganisha kwa nishati ya umeme nchi za Tanzania, Kenya, Ethiopia na Zambia.

Wabunge wa kamati hiyo walitembelea mradi huo kujiridhisha maendeleo yamefikia wapi kwasababu mwaka jana kulijitokeza changamoto kadhaa ikiwamo ya wafadhiri waliokuwa wameahidi kutoa fedha kujitoa na hivyo kuathiri mradi na wakati huo serikali ilikuwa imeshatoa Dola za Marekani milioni 400 kujenga miundombinu.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema katika utekelezaji wa mradi huo TANROADS wamepandisha gharama za usafirishaji wa mizigo wakati tayari mkataba ulishasainiwa jambo ambalo linasababisha kuongezeka kwa gharama za mradi na hivyo kuwapa mzigo Watanzania.

Alisema kwa upande wa TRA, vifaa ambavyo havitakiwi kulipiwa kodi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo serikali iwe inafuatilia na wanatekeleza kwa wakati kwani kumekuwa na tatizo la kuchelewesha kutoa vibali na kusababisha mkandarasi kusimama kuanza kazi jambo ambalo linawaumiza na kuwaingiza hasara Watanzania.

Hasunga alisema kamati yake imejifunza kwamba miradi mingi inayotekelezwa hapa nchini inachukua muda mrefu kukamilika kwa wakati kuliko muda unaokuwa umewekwa kwenye mikataba.

"Tunataka mfano ujenzi wa 'substation' ya Shinyanga ambayo mmetueleza mtaujenga kwa miaka mawili tunataka ndani ya muda huo uwe umekamilika ikizidi hapo gharama zitaongezeka, kwa hiyo serikali ihakikishe inatoa fedha mapema kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo," alisema.

Naye Mbunge wa Masasi, Geofrey Mwambe, alisema inashangaza TANROADS inaongeza tozo mbalimbali ambazo zinakwamisha miradi ya serikali kitu ambacho hakiingii akilini na TRA inatoza kodi ya VAT kwa vifaa ambavyo vinatakiwa visamehewe kwenye miradi ambayo ni ya serikali .

Aidha, alihoji suala la gharama za umeme utakaopatikana baada ya utekelezaji wa mradi huo kwani serikali haijawahi kufanikiwa inapoahidi upatikanaji wa umeme kwa gharama nafuu.

Mratibu wa KTPIP, mhandisi Peter Kidadye, alisema wakati wa utekelezaji wa mradi huo wamejifunza kutokana na changamoto zilizojitokeza kwenye suala la kodi na kusababisha kulipa fidia makandarasi kutokana na kuchelewa kuanza kwa mradi kwa sababu ya mgogoro wa kodi.

Alisema tatizo hilo la utozaji wa kodi lilijitokeza kwa Tanzania pekee wakati nchi ya Kenya hakukuwa na tatizo kutokana na utaratibu mzuri waliouweka kwenye utekelezaji wa miradi inayojengwa na serikali.

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Mhandisi Dk.Cosmas Masawe, aliwaeleza wabunge hao kwamba TRA na TANROADS wamekuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi ya umeme.

Dk.Masawe alishauri sheria kinzani zirekebishwe ili zisaidie kuendeleza niradi kwa gharama nafuu na pia wabunge wasaidie malipo ya awali kwa makandarasi yafanyike mapema kwa ajili ya kujenga kituo cha kusafirisha umeme Shinyanga.



# Makada 25 wa CCM wajitokeza kuwania uongozi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VITA ya kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, imepamba moto ambapo zaidi ya makada 25 wamejitokeza kuchukua fomu za kuwania nafasi hiyo ikiwa ni siku ya tatu tangu zilipoanza kutolewa.

Nafasi hiyo ilibaki wazi baada ya aliyekuwa anaishikilia kwa takribani miezi 11, Dk. Stephen Mwakajumilo kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara.

Akizungumza na wandishi wa habari jana, Kaimu Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Clemence Mponzi alisema fomu zilianza kutolewa Novemba 12 mwaka huu na mwisho itakuwa Novemba 26 mwaka huu saa 10:00 jioni.

Alisema mpaka juzi jioni makada 21 wa chama hicho walikuwa wamejitokeza kuchukua fomu hizo huku wanawake wakiwa ni watatu na kwamba wengine wanaendelea kujitokeza.

"Leo ni siku ya pili ya uchukuaji wa fomu, tunasubiri siku ya mwisho ndio tutajua ni wangapi watakuwa wamechukua fomu hizi, tunawaomba makada wa chama chetu wanaowiwa kugombea nafasi hiyo kuja kuchukua fomu hizi, kujaza na kurudisha kabla ya Alhamisi saa 10:00 jioni," alisema Mponzi.

Alisema fomu hizo zinatolewa bila malipo ya aina yoyote kutokana na maiongozo ya chama hicho na hivyo wanachama wote wenye sifa wajitokeze kuomba nafasi hiyo.

Mponzi alisema majina ya makada wote waliojitokeza kuchukua fomu hizo yatawekwa wazi siku ya mwisho baada ya uchukuaji wa fomu hizo kufungwa.

Miongoni mwa wanachama wa chama hicho ambao wameshachukua fomu hizo ni pamoja na aliyewahi kushika nafasi hiyo, Mchungaji Jacob Mwakasole ambaye alishika nafasi hiyo kwa miaka mitano.

Akizungumza baada ya kuchukua fomu hiyo, Mwakasole alisema aliamua kuchukua nafasi ya kuwania nafasi hiyo kwa mara ya pili kwa maelezo kuwa alikuwa benchi kwa mwaka mmoja pekee na kwamba hakuondoka kwa kashfa.

Alisema chama hicho ni kikongwe na kinafuata misingi ya demokrasia na kila mwanachama wa chama hicho mwenye sifa anastahili kuchukua fomu za kuwania nafasi hiyo.

"Mimi lengo lengu la kuwania nafasi hii ni kwamba nataka kukiimarisha zaidi chama na kuhakikisha siasa za chama chetu kinaendelea kushamiri, vilevile maono yangu ni kutaka kukiimarisha zaidi chama chetu," alisema Mwakasole.

Alisema kwa muda aliopumzika ana uhakika chama bado kipo imara huku akisisitiza kuwa alikuwa bado ni kada mwaminifu kwa chama hicho tawala.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akizungumza na Balozi wa Marekani nchini, Michael Battlema aliyekuwa mkoani humo jana, kwa lengo la kuangalia fursa mbalimbali ambazo serikali ya nchi hiyo inaweza kushirikiana na Tanzania zikiwemo za kwenye sekta ya kilimo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC ahimiza utoaji elimu matumizi sahihi ya mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera amewataka wazalishaji na wasambazaji wa mbolea kushirikiana na maofisa ugani kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao.

Homera alisema hayo jana kwenye uzinduzi wa ghala la kuhifadhia mbolea la kiwanda cha kuzalisha mbolea cha ITRACOM kilichopo jijini Dodoma.

Ghala hilo lipo katika eneo la Mafiati jijini Mbeya na litatumika kusambaza mbolea katika mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo inaongoza nchini kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo ya chakula.

Homera alisema wakulima wengi hawajui matumizi sahihi ya mbolea hali inayosababisha tija ndogo kwenye kilimo hivyo wanahitaji kuelimishwa ili wajue namna ya kutumia mbolea kwa usahihi.

"Serikali yetu imeweka maofisa ugani kila mahali lakini peke yao hawawezi kutoa elimu ya matumizi ya mbolea, hivyo niwatake wazalishaji kushirikiana na maofisa ugani kuanzia ngazi ya kata kuweka semina mbalimbali za wakulima kwa ajili ya mafunzo ya matumizi ya mbolea," alisema Homera.

Aidha, Homera aliwataka wakulima kujiandikisha kwa wingi ili kupata mbolea kwa bei ya ruzuku na kubainisha kuwa mpaka sasa zaidi ya wakulima 2,000 wameshajiandikisha kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku na kuwahakikishia mbolea hiyo kuwafikia wakulima wote.

Alisema wameshaanza kupima afya ya udongo kwenye baadhi ya vijiji na kuongeza kuwa kwa mwaka huu wanatarajia kutumia zaidi ya tani 82,000 kutoka tani 70,000 zilizotumika mwaka jana.

Mkurugenzi wa biashara na masoko kutoka kampuni ya Intracom, Dk. Keneth Masuki aliwahakikishia wakulima nchini kuwa changamoto ya upatikanaji wa mbolea itapungua kutokana na ongezeko la uzalishaji wa tani milioni moja kwa mwaka ingawa mahitaji kwa wakulima ni tani 700,000 pekee.

Dk. Masuki alisema wanampango wa kufunga mashine tano za uzalishaji wa mbolea katika kiwanda chao zitakazoongeza uzalishaji hadi tani 1,000,000 kwa mwaka na kukidhi mahitaji ya watumiaji.

# Viongozi wa dini wakemea ukatili wa wanawake, watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VIONGOZI wa dini mkoani Njombe wametakiwa kutumia nyumba za ibada kuhubiri amani na kukemea maovu ili kupunguza wimbi la matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwemo ubakaji.

Wito huo ulitolewa mkoani hapa na Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa kwa niaba ya Naibu Waziri wa TAMISEMI, Dk. Festo Dugange katika harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya bima ya afya kwa zaidi ya watoto yatima 600 na wenye ulemavu wa viungo wa kituo cha INUKA kilichopo wilayani Wanging'ombe kinachoendeshwa na Kanisa Katoliki.

Kasongwa alisema matukio yanayoendelea mkoani Njombe yanatisha na hayaleti afya kwa jamii kwani mbali na ukatili huo pia ripoti iliyotolewa na Rais siku chache zilizopita imebainisha Mkoa wa Njombe una ongezeko kubwa la mimba za ututoni ambao ni ukatili pia.

"Tunapata changamoto moja tu watu wa Njombe tunamjua Mungu lakini watu wa Njombe tunaongoza kwa matukio ya kutisha, matukio ya ukatili yani tunaongoza kwa matukio ya ovyo ovyo maana lazima tufike mahali tuongee ukweli," alisema Kasongwa.

Katibu wa kanisa hilo, Padri Athanas Mgimba alisema kituo cha viungo na yatima INUKA kilianzishwa kutokana na ongezeko la watoto wenye mahitaji maalumu wakiwemo wanaotokana na wazazi wao kukumbwa na ukatili pamoja na kutelekezwa.

"Tumeona kuna wagonjwa wengi ambao jamii imeshindwa kuwahudumia kwa mfano wanaopata kiharusi, wanaozaliwa na ulemavu kama miguu, wanapata ajali wanashindwa kunyoosha viungo," alisema Mgimba.

Mwenyekiti wa walezi wa Kwaya ya Mtakatifu Mbaga Tuzinde, Deogratias Mtewele alisema kupitia uinjilishaji waumini wanapata elimu ya kukabiliana na vitendo vya ukatili pamoja na mahubiri mbalimbali.

"Watoto hawa yatima wamepatikana katika mazingira tofauti tofauti kuna wale ambao walikuwa wanafanyiwa ukatili wazazi wao bado wapo wazima lakini wapo jela wanatumikia hukumu kutokana na matukio ya ukatili," alisema Mtewele.

Kwa upande wao waumini wa kutoka katika maeneo mbalimbali mkoani Njombe akiwemo Matrida Mwinuka na Francis Manga walisema wimbi la watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu linapaswa kuungwa mkono na kila mtanzania kwani adha imekuwa kubwa.





## Serikali kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuipa kipaumbele sekta ya michezo hususani michezo jumuishi ili kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu kujumuika pamoja.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyasema hayo katika hutuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla wakati akifungua warsha ya kimataifa kuhusu shule na michezo jumuishi visiwani hapa.

Alisema kuwepo na michezo jumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kutasaidia kukuza na kuhuisha ushiriki wa watu wenye ulemavu hususani ulemavu wa akili kwenye mashindano ya michezo ndani na nje ya nchi.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa eerikali zote mbili kwa kutambua umuhimu wa michezo zimeamua kuipa kipaumbele sekta ya michezo kwa kuhakikisha nchi inakuwa na viwanja vyenye hadhi ya kimataifa sambamba na kuboresha viwanja vya michezo shuleni.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa michezo serikali zote mbili zimewapa fursa watu wenye ulemavu na kuwawezesha kushiriki katika mashindano ya kimataifa yanayofanyika nchi mbalimbali duniani, kwamba serikali zitaendelea kusimamia na kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata fursa ya kujitangaza ndani na nje ya nchi.

Naye Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita alisema wataendelea kutoa ushirikiano katika kuhakikisha kuwa michezo jumuishi inapewa kipaumbele ili kutoa nafasi kwa watu wenye ulemavu wa akili kushiriki katika michezo ndani na nje ya nchi.

Waziri Tabia aliitaka serikali kuangalia kwa ukaribu uwezekano wa kuongeza bajeti katika fungu la michezo kwa mwaka wa fedha ujao ili kutoa nafasi kwa watu wenye ulemavu kushiriki katika michezo na kuomba kuangaliwa kushiriki katika sherehe za mapinduzi.

Raisi wa michezo ya Olimpic Afrika, Charles Nyambe, alisema kushiriki katika michezo ya olimpic kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wakiwemo wenye ulemavu wa akili kumewasaidia wanafunzi hao kukua kiakili na kimaarifa jambo ambalo linatoa matokeo chanya katika mashindano wanayoshiriki.

# Serikali yajinasibu kuandaa mazingira bora ya ufundishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuchukua jitihada za kuandaa mazingira bora ya ufundishaji wa wanafunzi ikiwemo kupata chakula wakiwa shuleni.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam wakati akisoma hutuba ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah katika uzinduzi wa mwongozo wa ulishaji wa chakula katika shule za maandalizi na msingi Zanzibar.

Alisema wanafunzi wengi hushindwa kujifunza kwa ufanisi kwa sababu wanakosa mlo (chakula) kwa muda mrefu wakiwa shuleni, kwamba jambo hilo husababisha wanafunzi wengi kuacha masomo, kuwa na matokeo mabaya na kushindwa kukabiliana na masomo. "Jitihada hizi zimewaibua washirika wetu Table for two international (TFT) kutoka Japan wakaamua kwa mapenzi yao makubwa kuwasaidia wanafunzi kwa kuwapatia chakula"alisema.

Alisema mradi wa Home Grown School Feeding unalenga kuwasadia wanafunzi wanaoishi katika maeneo tengefu na yenye mazingira magumu ambayo mara nyingi yanakuwa na changamoto za kujifunza.

Alisema mradi huo umeanza mwaka 2014 kwa kipindi cha majaribio katika Wilaya ya Kaskazini A Unguja na Micheweni Pemba zikiwa na jumla ya shule tisa, lakini mradi huo uliendelea kuwahudumia wanafunzi katika maeneo mingi mpaka kufikia shule 36.

"Kwa sasa tupo katika mchakato wa kuongeza shule sita. Jumla ya wanafunzi wanaonufaika na mradi mpaka kufikia Septemba mwaka huu ni 20,807 na malengo ni kufikia shule 50 ifikapo mwaka 2025" alisema.

Aidha, alisema lengo la mradi ni kuinua hali ya ujifunzaji wa wananfunzi kwa kuandaa mazingira rafiki pamoja na kuongeza uandikishaji wa wanafunzi, kuimarisha mahudhirio na kuongeza ufaulu, kujenga tabia bora, uhamasishaji vyakula vyenye virutubisho, kuimaridha afya za wanafunzi na kuongeza uzalishaji na kipato cha wakulima wadogo.

Hata hivyo alisema mradi huo umesaidia kuyafikia malengo yake na wananfunzi wengi wamepata fursa ya kusoma, kubaki shule kipindi chote cha masomo, kufaulu kwa kiwango cha juu na kuimarisha afya zao.

Alisema pamoja na umuhimu wa miradi ya ulishaji wa chakula katika shule bado kulikuwa na upungufu wa miongozo ya ulishaji wa chakula na ndipo wadau walitumia fursa kulisha watoto bila ya kufuata utaratibu maalumu na wakati mwengine kusababisha madhara yanayoonekana na yasioonekana.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdallah Said, alisema kuwa mtoto anahitaji kuandaliwa mazingira bora ya kupata elimu akiwa tangu mdogo ili kuwa na ufahamu mzuri na kufaulu masomo yake.

Alisema ulaji wa chakula bora kwa wananfunzi kutawajenga kuwa na afya ya mwili na kiakili na kupelekea kufanya vizuri katika masomo yao.

Hivyo, aliwataka wazazi na walenzi kujenga maadili ya watoto tangu akiwa wadogo ili baadae kuwa na viongozi wazuri wenye kuzingatia maadili.

Mkurugenzi wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sara Gibson alisema Serikali ya Zanzibar ina dhamira mzuri katika kuhakikisha watoto wanapata elimu inayofaa na kuipongeza serikali kwa hatua hiyo.

Alisema WFP itaendelea kuisaidia serikali katika mipango yake na lishe bora ina mchango mkubwa katika kuinua kiwango cha elimu, hivyo ni muhimu wanafunzi kupatiwa lishe bora.




Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam (katikati), akiwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khamis Abdallah (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Elimu Msingi na Maandalizi wa wizara hiyo, Fatma Mode (kushoto), Mkuu wa Kitengo cha Lishe wa Shirika la Mpango wa Chakula Dunia (WFP) nchini, Vera Lugutual (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mkazi wa WFP Tanzania, Sara Gidison wakionyesha kitabu cha mwongozo wa utoaji wa chakula mashuleni, baada ya kuuzindua mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wavuvi wapewa elimu kuhusu athari ya uvuvi haramu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Divisheni ya Usarifu wa Mazao ya Baharini kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Ali Khamis Shafi amewataka wavuvi kuachana na uvuvi haramu kwa sababu ni chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira na ikolojia ya baharini. Akitoa elimu ya athari za uvuvi haramu katika Soko la Malindi Mjini Unguja jana, alisema uharibifu wa ikolojia na mazingira husababisha kupungua kwa idadi ya watalii na kupotea kwa pato la taifa.

Alisema wavuvi wanapaswa kufuata Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2010 ambazo zinaelekeza uvuvi unaokubalika kisheria kwa lengo la kuwa na uhakika wa soko la ndani na nje ya nchi ili kuleta matumaini mazuri ya usalama wa afya ya mlaji wa samaki.

Shafi alisema ili samaki awe na ubora kwa mlaji lazima mvuvi atumie njia bora za kuhifadhi samaki ili kuepusha madhara mbalimbali yanayohitokeza katika samaki.

Aidha, alisema suala la usafi katika soko ni jambo la lazima kutokana na wateja wakuu katika masoko ni watalii, hivyo lazima kudumisha usafi ili kukuza biashara hiyo ya samaki kwa soko la ndani na la kimataifa.

Pia, aliwataka wavuvi kubadilika kutokana na jamii ya ukanda wa pwani ni wale waliozungukwa na bahari na hutegemea kwa kiasi kikubwa shughuli za uvuvi ili kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao.

Naye Sheha wa Shehia ya Malindi, Hassan Masoud Ali alisema yupo tayari kushirikiana katika kutoa elimu kwa wavuvi wanaofanya shughuli zao katika Shehia ya Malindi kwa ajili ya maendeleo kwa taifa.

Akizungumza kwa niaba ya wavuvi na wachuuzi wa kambi ya wavuvi ya Malindi, Issa Abubakar Said alisema wapo tayari kubadilika kutokana na athari kubwa iliojitokeza baharini juu ya matumizi ya sumu.

Aidha, alizitaka taasisi husika kuwawekea mwongozo maalumu utaonesha samaki anavohitajika kuhifadhiwa baada ya kuvuliwa hadi kufika sokoni kwa lengo la kuikuza biashara ya samaki ili kumkomboa mvuvi kiuchumi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**HELENA JAMES,** Anatangaza kupotea kwa Cheti chake cha darasa la saba kilichotolewa na Baraza la Mitiahani la Taifa kupitia shule ya Secondary Yeriko Primary Mwaka 2009, Cheti cha Kidato cha Nne chenye **index no S 3843-0033** kilichotolea na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Secondari A.M SHABIBY Mwaka 2013, Cheti cha Kidato cha Sita chenye index no **S 0430-0563** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari UWEMBA Mwaka 2016, Cheti cha chuo chenye no **BED PPM 00002042** Kilichotolewa Na CHUO CHA DODOMA Mwaka 2019. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/8625/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**BARAKA SAMWEL MANYANDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC 652 DFD.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/6806/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUMAA KOMBO KOMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA PREMIO** yenye usajili namba: **T 197 DDY, CHASSIS** NAMBA: **ZZT2400070759** na ENGINE NAMBA: **1ZZT16665457.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chocha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/6100/2023**

**THE REGISTRATION DOPCUMENTS ACT**
**(CAP.117)R.E 2002.**
**DEEDPOLL.**

**BY THIS DEED,SAMWEL KASOBANA POKELA** OF P.O.BOX 14 **SONGEA,HEREBY BY wholly,** absolutely and utterly renounce,relinquish and abandon the use my former names of **SAMWEL KABOSANA POKELA**,and in lieu thereof to assume and adopt the names of **SAMWEL KASOBANA POKELA.**
**FOR THE PURPOSE** of evidence of such determination,Ihereby **DECLARE** that at all times hereinafter in all records,deed,documents and other writings and in all action,proceedings as well as in all public and prive dealings and transaction and creations and creations whatsoever use and subscribe the said names of **SAMWEL KASOBANA POKELA** as my name in lieu of and in substitution for my former name of **SAMWEL KABOSANA POKELA.**
**AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the datehereof to designated,describe and address me by the adopted names of **SAMWEL KASOBANA POKELA.**
I make this declaration consciounsly believing the same to be true in accordance with the provision of Oaths and Statutory Act, 1966.

SIGNED and DELIVERED by the said
SAMWEL KASOBANA POKELA
Who is known to me personally
This Day of 12 July 2023
BEFORE ME:
Name: Happiness Shelembi
Signature:
Postal address:
Qualification:



DEPONENT

HAKIMU WA MAHAKAMA MAHAKAMA YA MWANZO SONGEA MJINI SONGEA

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**IN THE DISTRICT COURT (DISTRICT DELEGATE OF MANYONI DISTRICT**
**AT SINGIDA**

**PROBATE AND ADM, CAUSE NO. 9 OF 2023**

**And**

**In the matter of Application for Grant of Letters of the estate of late PEM MALOGO MLANJIZE – (DECEASED)**
**And**

**In the matter of Application for Letter of Administration without will by**
**MODESTER PIASON MLANJIZE – PETITIONER**
**(Section 33, Rule 84)**

**BE IT KNOW** that letter of administration of the properties and credits of the late **PEM MALOGO MLANJIZE** who died at Nkonko – Manyoni o the 29th of August, 2023 is **HEREBY GRANTED TO MODESTER PIASON MLANJIZE – PETITIONER** the daughter of deceased having undertaken to administer the said properties and credits and to make a fully and true inventory of the said properties and credits and exhibit the same in this court within six months from the day of this grant or within such further time as the court may from time to time appoint, and to render to this court a true account of the said properties and credits within one year from the same date or within such further time as the court my from time to time appoint.

**Dated at Singida this 3rd day of November, 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE MANYONI

**PAVESEAL LIMITED**
**COMPANY NUMBER 97126**
**PLOT NUMBER 202/1, NYERERE ROAD,**
**CHANG'OMBE 'B' STREET, CHANG'OMBE WARD,**
**TEMEKE DISTRICT, DAR ES SALAAM**
**P.O. BOX 4 DAR ES SALAAM, TANZANIA**

## NOTICE OF THE FINAL GENERAL MEETING

Notice is hereby given that, a final meeting of the above-named company will be held on 15th December, 2023 at 10:00 am, Plot number 202/1, Nyerere Road, Chang'ombe B Street, Chang'ombe Ward, Temeke District, Dar es Salaam region.

**Agenda:**
- To receive the Winding up report from the liquidator
- To lay down the accounts of the Company
- To finalize queries from creditors, if any
- Any other Businesses

By Order of the Company Liquidator.

**HAMZAALI AMIRALI PATWA**
**H. A. PATWA & CO.**

**Dated at Dar es Salaam this 14th November, 2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI ...230... LA 2022**
**PATRICE F. SANGAWE.........MUOMBAJI/WAOMBJI**
**DHIDI YA**
**HUSEINI ABDALLAH SEIFU.........MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**HUSEIN ABDALLAH SEIFU**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**PATRICE F. SANGAWE** Amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 7/12/2023 saa 3.00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh J.W. SILLAH Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 Mwezi ..10..., 2023

**FOMU MADAI - 3**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 1698/2023**
**Jina la Mdai: WAKEELAH ALLIYAH**
**Jina la Mdaiwa: LUTEGANO D. MPONELA**
**KUITWA SHAURINI**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: LUTEGANO D. MPONELA**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii terehe 14 Mwezi wa 11 Mwaka 2023 saa 9:00 asubuhi mbele ya Mh. MAYAYA kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO**: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 Mwezi wa 11 Mwaka 2023.

HAKIMU

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.140 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late DAUSEN ANAEL TOWO of Chang'ombe, Chang'ombe Juu Ward within Dodoma City Council**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY DONATHA CHRISTOPHER KESSY.**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 21 Day of 11, 2023
Dated at Dodoma this 14 Day of 11, 2023

..............................................
**PETITIONER**
Presented for filling this 14 Day of 11...........2023

..............................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**DRAWN AND FILED BY**
**PETITIONER**
**CHANG'OMBE JUU WARD**
**P. O. BOX 1249**
**DODOMA**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0745 700 710.*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

## HABARI KIMATAIFA

# Raia wa Nigeria wazuiliwa kuingia Saudia

**LAGOS,** Nigeria

ZAIDI ya Wanigeria 177 waliokuwa wakisafiri na ndege kuelekea Saudi Arabia kwa ajili ya ibada ndogo ya hija (Umrah) katika mji wa Makka, wamerudishwa baada ya mamlaka ya Saudia kufuta viza zao wakiwa safarini.

Hayo yalibainishwa jana na vyombo vya habari vya Nigeria, huku ikielezwa kuwa abiria 264, ambao walikuwa wameondoka katika miji ya Lagos na Kano ya Nigeria, walipokea viza na kufanyiwa uchunguzi mkali kabla ya kupanda ndege.

**Hata hivyo, ilibainishwa kuwa baada ya Balozi wa Nigeria kuingilia kati Saudi Arabia iliruhusu raia 87 pekee kuingia nchini humo, huku waliobaki 177 wakirejeshwa nyumbani.**

Ripoti zilieleza kuwa viza zote za raia hao zilifutwa wakiwa angani, na kwamba walipofika, mamlaka ya Saudia ilikataa kuwaruhusu kuingia na kuamuru shirika la ndege la Air Peace la Nigeria kuwarejesha nyumbani Nigeria.

Aidha, ilielezwa kuwa hadi jana Mamlaka ya Saudia haikuzungumza chochote kuhusu suala hilo.

Abiria waliokumbwa na mkasa huo walipozungumza na vyombo vya habari, walieleza kuwa walishangazwa na taarifa za kukataliwa kwa viza zao baada ya kushuka Saudia, huku wakidai kwamba walikidhi vigezo vyote vya kuingia nchini humo.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa baada ya Balozi wa Nigeria kuingilia kati Saudi Arabia iliruhusu raia 87 pekee kuingia nchini humo, huku waliobaki 177 wakirejeshwa nyumbani.

Ripoti za vyombo vya habari vya Nigeria zinasema wengi wa abiria hao walikuwa wamesafiri hadi Saudi Arabia kutekeleza ibada ndogo ya Hija (Umrah), kuhiji katika mji mtakatifu wa Kiislamu wa Makka.

BBC"Nilikuwa katika usingizi mzito kwa sababu sikuwa nimelala siku zilizopita," aliambia BBC. **BBC**



Vifaru vya Jeshi la Israel vikiwa vimeenea katika maeneo ya Gaza kutokana na vita vinavyoendelea. **PICHA: MTANDAO**

# Hospitali ya Al Shifa -Gaza yazungukwa na vifaru

**GAZA,** Palestina

MAOFISA wa Wizara ya Afya Ukanda wa Gaza walisema Jeshi la Israel limeweka vifaru nje ya hospitali ya Al Shifa, ambayo ndio kituo kikuu cha matibabu katika jiji la Gaza.

Israel ilisema chini ya hospitali hiyo kuna mahandaki yanayotumika kama makao makuu ya wapiganaji wa Hamas wanaotumia wagonjwa kama ngao, huku Hamas ikikanusha madai hayo.

Kabla ya kuizingira hospitali hiyo ilielezwa kuwa vikosi vya Israel vilishambulia kusini mwa Gaza, na kwamba takribani watu 13 waliuawa baada ya vikosi hivyo kuyalenga makazi yao katika mji wa Khan Younis.

Katika hatua nyingine ilibainishwa kuwa Israel inasimamia utaratibu wa kupelekwa Gaza mashine za kuwatunza watoto njiti, katika hatua ya kuwezesha kuhamishwa watoto wachanga kutoka hospitali hiyo iliyozingirwa.

Msemaji wa wizara ya afya ya Gaza Ashraf Al-Qidra ambaye alikuwa ndani ya hospitali ya Al Shifa, alisema wagonjwa 32 walifariki dunia katika siku tatu zilizopita, wakiwemo watoto watatu wachanga, huku ikielezwa kwamba kwa sasa kuna wagonjwa 650 ndani ya hospitali hiyo.

Mkurugenzi wa hospitali ya Al-Shifa Mohammad Salmiyah, alisema watu 179, wakiwemo watoto na wagonjwa waliofariki katika kitengo cha wagonjwa mahututi, wamezikwa kwenye kaburi la pamoja hospitalini hapo.

Katika matamshi yake ya kwanza tangu kuripotiwa kwa vifo vya wagonjwa katika hospitali ya Al Shifa, Rais wa Marekani Joe Biden alisema hospitali lazima zilindwe.

Kundi la kijeshi la Hamas linalofahamika kama Al-Qassam Brigades linasema liko tayari kuwaachia hadi wanawake na watoto 70 wanaoshikiliwa Gaza, kwa kubadilishana na usitishwaji mapigano kwa siku saba katika vita hivyo.

Msemaji wa Al-Qassam Abu Ubaida, alisema waliwaambia wapatanishi wa mzozo huo, Qatar kuwa wanaweza kuwaachia huru mateka 50 hadi 70 kutokana na ugumu kuwa wanashikiliwa na makundi tofauti.

Israel ambayo imeizingira Gaza, ilikataa mpango wa usitishwaji kamili wa mapigano, ikihoji kuwa Hamas inaweza kutumia fursa hiyo kujipanga upya, lakini imeruhusu usitishwaji vita kwa nyakati fulani kwa misingi ya kiutu, ili kuruhusu chakula na bidhaa nyingine kuingia Gaza na kuondoka kwa raia wa kigeni.

Ilielezwa kuwa katika ukingo unaokaliwa wa Magharibi, karibu Wapalestina wanane wameuawa na vikosi vya Israel, huku Wizara ya Afya ya Palestina ikisema watatu kati ya hao waliuliwa katika shambulizi la droni ya Israel.

Jeshi la Israel na polisi wamesema vikosi vyao vilivyotumwa katika eneo la Tulkarm kuwakamata washukiwa wa kigaidi, walishambuliwa na wakawauwa wapiganaji wa Kipalestina katika vurugu zilizozuka.

Aidha, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya masuala ya kibinadamu (OCHA) ilisema watu wengine 200,000 wamekimbia kaskazini mwa Gaza tangu Novemba 5, mwaka huu. **DW**

# Biashara fedha za kigeni kusitishwa Malawi

**LILONGWE,** Malawi

WIZARA ya Fedha ya Malawi imesema itaanza kuzuia biashara ya fedha za kigeni na kufanya msako dhidi ya wafanyabiashara wa magendo, baada ya kushuka thamani ya sarafu yake.

Kwa mujibu wa shirika la habari Reuters, nchi hiyo ya kusini mwa Afrika ilishusha thamani ya sarafu ya Kwacha kwa asilimia 30 dhidi ya dola ya Kimarekani siku chache zilizopita, ikisema kwamba hatua hiyo ni muhimu katika udhibiti wa soko la fedha.

Waziri wa Fedha wa Malawi Simplex Banda, alisema kwamba mauzo ya fedha za kigeni kwenye benki pamoja na taasisi nyingine za kifedha hayatavuka dola 2,000 kuanzia sasa. Na kwamba polisi wataanza kufanya misako dhidi ya wafanyabiashara haramu wa fedha.

Pia alisema kwamba Malawi imeshauriana na Benki ya Dunia pamoja na mashirika mengine ya kimataifa kuhusu kuongeza misaada kwa watu masikini kupitia progam ya serikali ya 'Social Cash Transfer' (SCTP) ili kuwalinda watu masikini dhidi ya athari za kushushwa kwa thamani ya sarafu, wakati pia kukiwa na mashauriano na mashirika ya wafanyakazi kuongeza mishahara.

Inaelezwa kuwa hiyo ni mara ya pili kwa Malawi kushusha thamani ya sarafu yake katika miaka ya karibuni, mara ya kwanza ikiwa mwezi Mei 2022. Huku hatua hiyo ikiibua malalamiko makali kutoka kwa baadhi ya wakazi, ambao pia wanapanga kuandamana.

Ilibainishwa kuwa bei za mafuta na umeme pia zilipandishwa huku waziri wa fedha akitetea hatua hiyo kwamba itasaidia kuimarisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa, pamoja na kuvutia wawekezaji wa kigeni. **VOA**

HABARI MICHEZO

# KIBU AMSAIDIA KIPA TABORA UTD KUMSHUSHA DIARRA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa Simba, Kibu Denis, aliyefunga bao la kufutia machozi kwenye mechi ya watani wa jadi dhidi ya Yanga, timu yake ikikubali kipigo cha mabao 5-1, Novemba 5, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, amesababisha kipa wa Yanga, Djigui Diarra, kuenguliwa kuwa kinara wa kucheza michezo mingi bila kuruhusu bao (clean sheets), hadi kufikia raundi ya tisa ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Diarra ambaye kwa muda mrefu alikuwa akiongoza kwa 'clean sheets' kwa sasa amezidiwa na Kipa wa Tabora United raia wa Nigeria, John Noble.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu za Michezo cha Nipashe, Noble amefikisha 'clean sheets' tano na kumuacha Diarra akibaki na nne, ambapo kama raia huyo wa Mali asingefungwa bao kwenye mechi hiyo dhidi ya Simba, naye angekuwa na 'clean sheets' tano, na kuwa mmoja wa vinara wa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao.

Noble amepata 'clean sheets' kwenye mechi ambazo timu yake ilitoa suluhu zote bila kufungana.

Alisimama langoni, timu yake ikitoa suluhu dhidi ya Singida Fountain Gate, Coastal Union, Kagera Sugar na Geita Gold ikicheza ugenini na nyingie dhidi ya KMC nyumbani, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Diarra anakamata nafasi ya pili ambapo 'clean sheets' zake nazo alizipata kwenye mechi dhidi ya JKT Tanzania, Yanga ikishinda mabao 5-0, ikichapa Namungo bao 1-0, Geita Gold mabao 3-0, na katika mchezo dhidi ya Singida Fountain Gate, wakishinda 2-0.

Diarra hakukaa langoni kwenye mechi ya ufunguzi, Yanga ikishinda mabao 5-0, ambapo Metacha Mnata alikuwa langoni na mchezo wa Jumatano iliyopita Uwanja wa Mkwakwani Tanga iliposhinda bao 1-0, akisimama Aboutwalib Mshery.

Kipa mwingine wa kigeni, Mkongomani Ley Matampi wa Coastal Union ana 'clean sheets' tatu, sawa na Mghana Adrisu Abdulai wa Azam FC, huku kipa Mtanzania pekee aliyechomoza ni Daniel Mgore wa Dodoma Jiji akiwa nazo tatu pia.

MAANDALIZI...



Wachezaji wa Simba wakiendelea na mazoezi ya viungo gym, Dar es Salaam juzi, kabla ya kuhamia uwanjani kujiandaa na mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast itakayopigwa Novemba 25, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: SIMBA**

# *Kocha Bara U-15 alia bahati, Z'bar yafuzu*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa timu ya Bara ya wavulana chini ya miaka 15, Maalim Salehe, amesema bahati ndiyo iliyoibeba Uganda hadi kupata ushindi wa mabao 2-1 juzi kwenye mechi ya nusu fainali ikipigwa Uwanja wa Njeru, Jinja nchin humo katika michuano ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati, CECAFA.

Wakati Bara ikiondolewa kwenye michuano hiyo, Zanzibar katika mechi ya baadaye, ilifanikiwa kutinga hatua fainali kwa kuiondosha Sudan Kusini kwa mikwaju 4-2 ya penalti, baada ya kwenda dakika 90 zikifungana bao 1-1, na sasa itakutana na Uganda katika mechi ya fainali itakayopigwa kesho kwenye uwanja huo.

"Mchezo ulikuwa nzuri sana na niliwaambia wachezaji wangu wacheze kwa nguvu, katika mechi ambazo Uganda wamepata upinzani basi ni mechi hii. Wamepata upinzani mkubwa sana, walikuwa wanaombea mpira uishe, nadhani dakika zingekuwa nyingi kidogo tungeweza kurudisha kwa sababu huku mwishoni tuliwashambulia sana, kikweli ni kwamba hatukuwa na bahati tu," alisema kocha huyo ambaye ni straika wa zamani wa Yanga, akipachikwa jina la Romario.

Mabao ya Uganda yalifungwa na Abubakali Walusimbe na Samuel Muburu, bao la Bara likifungwa na Feisal Juma.

Abdulhafidh Salmin aliifungia Zanzibar bao, huku Anur Loboro akifunga kwa upande wa Sudan Kusini na kusababisha timu hizo kwenda kwenye mikwaju ya penalti.

Mikwaju ya penalti kwa Zanzibar iliwekwa wavuni na Abdulhafidh Salmin, Mohamed Shaaban, Saleh Mbarouk na Mohamed Nassor, huku Lazarus Peter, George Laku na Victor Elizaya wakikosa penalti zao kwa upande wa Sudan Kusini, Ismail Mansuk Felix Marial wakiziweka kwenye kamba.

# India, Tanzania waandaa riadha

**Na Faustine Feliciane**

UMOJA wa India na Tanzania umeandaa mbio za riadha zitakazofanyika siku mbili kuanzia Desemba 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Srikanta Pradhan, alisema mbio hizo zitahusisha wakimbiaji ambao ni raia wa Tanzania na India.

Alisema wameandaa mbio hizo kuhakikisha wanadumisha umoja uliopo kati ya nchi hizo mbili ikiwamo wanariadha mbalimbali kubadilishana mawazo.

Alisisitiza kuwa mbio hizo pia zitahudhuriwa na mwanariadha mkongwe na Balozi wa Fit India, Milind Soman, ambaye alishaibua vipaji mbalimbali vya mchezo huo kuanzia hatua ya mitaa huko Mumbai, India.

Alisema, Soman ambaye kwa sasa ni mkufunzi wa mbio za riadha nchini India, atapata fursa ya kuzungumza na wanariadha mbalimbali kuhakikisha wanabadilishana uzoefu.

Alisema mbio hizo siku ya kwanza zitaanzia Dar es Salaam hadi Bagamoyo na siku ya pili zitaanzia Bagamoyo kurudi Dar es Salaam ambapo zitajumuisha jumla ya kilometa 120.

"Umoja wa India na Tanzania tumeandaa mbio za riadha ambazo zitafanyika kuanzia Dar es Salaam hadi Bagamoyo mkoani Pwani na baadaye zitatoka Bagamoyo kurudi Dar es Salaam ambapo tutakimbia kilometa 120, pia tutakuwa na mkongwe Soman ambaye hivi sasa ni mkufunzi wa mchezo huu na msanii wa filamu nchini India," alisema Balozi Pradhan.

Kwa upande wa Soman, alisema amefurahia sana kuja Tanzania na kushiriki katika mbio hizo.

"Ni fursa nzuri kwetu kutembelea Tanzania kuja kuiongoza timu itakayoshiriki mbio za riadha kwa pamoja ambapo tutaungana na Watanzania mbalimbali lengo likiwa ni kubadilishana uzoefu.

"Nimeshafanya safari kama hizi katika nchi mbalimbali ulimwenguni, sasa ni zamu ya Tanzania, kuhakikisha tunafikia malengo.

"Tunafurahi na tunajivunia kuwakilisha Ubalozi wa India nchini Tanzania kupitia mbio za riadha ninafikiri tutaacha alama kwa wenyeji," alisema Soman.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RISHARLISON, SANCHO SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na Brazil, Richarlison, 26, na winga wa Manchester United, Jadon Sancho, 23, wanawaniwa na klabu za Ligi Kuu ya Saudia. ***(Telegraph)***

### JUVE YAMTAKA SANCHO

KLABU ya Juventus pia ina nia ya kumsajili Jadon Sancho, lakini kwa mkopo huku wakitarajia United kumlipa sehemu ya mshahara wake. ***(Fabrizio Romano)***

### JAMES KUBAKI CHELSEA

MLINZI wa England, Reece James, 23, ameendelea kujitolea kikamilifu kwa Chelsea licha ya Manchester City na Real Madrid kuonesha nia ya kutaka kumsajili. ***(90min)***

### MABOSI UNITED WAKATAA

WAKUU wa Manchester United wanakataa kukutana na wakala kwani wanaamini kuwa wanajaribu kutafuta wateja kuchukua nafasi ya Erik ten Hag kama kocha pale Old Trafford. ***(ESPN)***

### MOSCARDO NA CHELSEA

KIUNGO wa Corinthians mwenye umri wa miaka 18, Mbrazil Gabriel Moscardo, ambaye amezivutia Arsenal na Barcelona, amesema Chelsea walikuwa na nia ya kumsajili msimu huu wa majira ya joto. ***(Talk sports)***

### MADRID YATAKA NYOTA

KLABU ya Real Madrid imewaongeza kiungo wa Ujerumani, Florian Wirtz, 20, mlinzi wa Uholanzi, Jeremie Frimpong (22) na mshambuliaji wa Nigeria, Victor Boniface, 22, kutoka Bayern Leverkusen kwenye orodha yao fupi ya uhamisho. ***(Football Transfers)***

### BARCA KUMUUZA RAPHINHA

BARCELONA bado inampango wa kumuuza winga wa zamani wa Leeds United, Raphinha, 26, msimu ujao, na wanatumaini klabu kubwa za Ulaya zitaweka dau la kumnunua mshambuliaji huyo wa Brazil. ***(Fichajes)***

### BAYERN YAMZUIA DAVIES

RAIS wa Bayern Munich, Herbert Hainer, amesema hawana nia ya kumuuza beki wa Canada, Alphonso Davies, 23, licha ya tetesi kwamba Real Madrid wanamtaka. ***(90 Min)***

### CANNAVARO ATAJWA NAPOLI

BEKI wa zamani wa Italia mzaliwa wa Naples, Fabio Cannavaro mwenye umri wa miaka 50, yuko kwenye orodha ya wale wanaopigiwa upatu kuchukua nafasi ya Rudi Garcia kama kocha mpya wa Napoli. ***(Fabrizio Romano)***

### MILITAO KUFUNGWA ZAIDI

REAL Madrid iko tayari kumuongezea mkataba mlinzi wa Brazil, Eder Militao, 25, hadi angalau 2028. ***(Mundo Deportivo)***

### MIKATABA MIPYA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imemuongezea mkataba wa miaka sita mshambuliaji wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, 19, sambamba na wachezaji wengine wanaolipwa fedha nyingi katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# OSIMHEN ATAJA KLABU MBILI ANAZOWEZA KUTUA ENGLAND

**NAPLES,** Italia

NYOTA wa Klabu ya Napoli, Victor Osimhen, amefichua kuwa alikuwa akimiliki jezi za klabu mbili za Ligi Kuu England, alipokuwa mdogo ambazo ni Manchester United na Chelsea.

**Osimhen amekuwa mmoja wa washambuliaji wa kutisha zaidi duniani katika miaka michache ya hivi karibuni.**

Raia huyo wa Nigeria aliwasili Ulaya na kujiunga na Klabu ya Wolfsburg ya Ujerumani mwaka 2017 baada ya kufanya vizuri kwenye Kombe la Dunia la Vijana wasiozidi umri wa miaka 17.

Kisha alipata kwenda kwa mkopo nchini Ubelgiji kabla ya mwaka mmoja baadye kuchukuliwa na Klabu ya Lille ya Ufaransa na kusababisha Napoli kulipa ada ya rekodi ya klabu ya euro milioni 70, ambayo inaweza kupanda hadi euro milioni 80 kwa huduma yake.

Baada ya kuimarika baada ya mwaka nchini Italia, Osimhen alifunga mabao 31 katika mashindano yote msimu uliopita huku Napoli ikitwaa taji lao la kwanza la Serie A tangu

**Nilipokuwa nakua, nilikuwa na jezi mbili, moja ilikuwa ya Chelsea na nyingine ya...**

mwaka 1990 wa siku za gwiji Diego Maradona.

Napoli walikuwa na matumaini ya kumsainisha Osimhen mkataba mpya, ingawa makubaliano hayajakamilika kwa sababu kadhaa na uhusiano wake na klabu hiyo unaaminika kudorora kutokana na video iliyowekwa kwenye chaneli rasmi za klabu ikimdhihaki.

Licha ya kurejea na mabao sita katika mechi nane za Serie A msimu huu kabla ya kukumbwa na jeraha, uvumi kuhusu kuondoka Napoli umeongezeka.

Maoni yake ya hivi karibuni kuhusu timu ambazo anaonekana kuzifuata akiwa mtoto zimechochea uvumi huo.

"Nilikuwa na jezi mbili, moja ilikuwa ya Chelsea na nyingine ya Manchester United," alifichua Osimhen katika kipindi kipya zaidi cha televisheni cha 'The Obi One Podcast' kinachoendeshwa na gwiji wa zamani soka wa Nigeria, John Obi Mikel.

Mikel ambaye ni kiungo wa zamani wa Chelsea alimwambia Osimhen: "Msimu ujao, najua utakuja Chelsea. Ninakuambia, nitakuwa wakala wa udalali huo. Mimi tutahakikisha hilo linafanyika. Tunamlilia mtu kama wewe...tangu Didier Drogba alipoondoka kwenye klabu."

'The Blues' wamekuwa wakivutiwa na Osimhen kwa muda mrefu na 90min iliripoti kwamba wanakusudia kusubiri kuona kama atasaini mkataba mpya na Napoli wiki zijazo.

Ili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, akubali mkataba huo, Napoli inaweza kuhitaji kujumuisha nyongeza kubwa ya mishahara na kifungu cha kuachiwa.

Msimu uliopita wa majira ya joto, Napoli walikuwa wakitaka hadi euro milioni 150 kumuuza Osimhen, lakini thamani yake itashuka kadiri mkataba wake wa sasa unavyokaribia kuisha mwaka 2025.

Manchester United walikuwa wakitaka kuwanunua Osimhen na Harry Kane kabla ya kumgeukia Rasmus Hojlund.

# TEN HAG AKINGIWA KIFUA MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

MABOSI wa Manchester United wamekataa kukutana na mawakala kwani wanaamini kuwa wanajaribu kuwatafutia wateja wao kuchukua nafasi ya Erik ten Hag, kwa mujibu wa ESPN.

Ten Hag alipunguza shinikizo kwenye nafasi yake kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Luton Town Jumamosi iliyopita katika mchezo wa mwisho wa United kabla ya mapumziko ya kimataifa ya Novemba hii.

Licha ya kupoteza mara tisa katika mechi 18 za msimu mpya, Mholanzi huyo anabaki kuaminiwa na viongozi wakuu wa klabu baada ya kumaliza nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu England na kushinda Kombe la Carabao msimu uliopita.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba wakuu wa United wamechanganyikiwa na majaribio ya mawakala kushinikiza makocha kuwania nafasi ya Ten Hag.

Mmoja wa wakala wa kocha mashuhuri, ambaye hayuko kazini, aliahirisha mkutano ulioratibiwa kwa sababu ya wasiwasi kwamba mazungumzo hayo yasingekuwa na matokeo chanya.

Mabosi wa United wanaamini kuwa kumekuwa na dalili za maendeleo katika kipindi cha wiki moja ambapo timu ya Ten Hag imezishinda Fulham na Luton kwenye Ligi Kuu, lakini walifungwa 4-3 na FC Copenhagen kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini inakubalika kwamba uwekezaji unaokuja wa Sir Jim Ratcliffe utaleta uhakika katika viwango vyote vya klabu mara tu utakapothibitishwa.

Ratcliffe, Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kemikali ya INEOS, anakaribia kukubaliana na ununuzi wa hisa asilimia 25 za klabu hiyo.

## Deco: Barca inamuunga mkono Xavi

**BARCELONA,** Hispania

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco, amesema Xavi Hernandez anabakia kuwa "kocha bora" wa klabu hiyo licha ya kushuka kwa kiwango cha timu hivi karibuni.

Xavi aliiongoza Barca kutwaa taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu uliopita - ambayo ilikuwa kampeni yake ya kwanza kamili kuinoa klabu hiyo baada ya kuchukua mikoba mwaka 2021- lakini matokeo ya mwaka huu yameongeza shinikizo kwenye nafasi yake.

Barca tayari wamepoteza pointi dhidi ya Getafe, Mallorca na Granada kwenye ligi, huku vipigo viwili katika mechi zao nne zilizopita, dhidi ya Real Madrid na Shakhtar Donetsk, vilisababisha ukosoaji mkubwa kwenye vyombo vya habari.

Timu hiyo ya Katalunya iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Alaves Jumapili, lakini kama ilivyokuwa kwa Real Sociedad wiki moja kabla, licha ya kushinda mechi hiyo, Xavi alikiri uchezaji ulikuwa wa kiwango cha chini kwa kile kinachotarajiwa klabuni hapo.

"Sina shaka kwamba Xavi ndiye kocha bora wa Barca," alisema Deco akiiambia Diario Sport juzi.

"Alikubali changamoto ya kuchukua nafasi katika wakati mgumu na yeye ndiye kocha kamili wa kutekeleza ujenzi tunaoendelea nao."

Xavi alichukua mikoba ya Ronald Koeman miaka miwili iliyopita akiwa na Barca nafasi ya tisa kwenye LaLiga na baada ya kupanda kwenye msimamo na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021-22, aliwaongoza 'Blaugrana' hao kutwaa taji lao la kwanza la ligi katika miaka minne msimu uliopita.







## Fabregas kocha mpya Como ya Italia

**ROME,** Italia

KIUNGO wa zamani wa Hispania, Cesc Fabregas, amechukua mikoba ya ukocha ya muda ya kuinoa timu ya Italia ya Serie B ya Como, klabu hiyo ilithibitisha Jumatatu.

Fabregas atachukua nafasi ya Moreno Longo kama kocha, baada ya Muitaliano huyo kushinda michezo 16 pekee kati ya 45 aliyoiongoza.

Kazi hiyo itakuwa alama ya kwanza ya ukocha kwa Fabregas mwenye umri wa miaka 36.

Kiungo huyo wa zamani wa Arsenal, Barcelona na Chelsea alistaafu kucheza soka Julai mwaka huu.

Fabregas alicheza mechi 17 katika ligi ya daraja la pili ya Italia akiwa na Como msimu uliopita kabla ya kuchukua nafasi ya kocha wa timu ya vijana ya klabu hiyo.

Como iko katika nafasi ya sita kwenye msimamo na itamenyana na Feralpisalo nyumbani Novemba 25, mwaka huu.

## Stars yatumia mashushushu kuisoma Niger

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Taifa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco,' amesema wamekuwa wakiifuatilia Niger kwa ajili ya kujua mbinu zao na aina yao ya uchezaji ili wajue wanawakabili vipi Jumamosi ijayo ugenini katika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu Kombe la Dunia 2026.

Tayari Taifa Stars ipo kambini jijini Dar es Salaam ikiendelea na mazoezi katika Uwanja wa JKT uliopo Kunduchi, kujiandaa na mchezo huo wa ugenini na kurejea nyumbani kuikaribisha Morocco katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo alisema karibuni wachezaji wote wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchini wamewasili, na mazoezi makali yanaendelea kuwaweka sawa wachezaji, huku tayari wakiwa wameshatuma watu kwa ajili ya kuendelea kuisoma Niger.

"Mazoezi yanaendelea vizuri, ushindani ni mkubwa na ni kitu kizuri kwetu sisi, kila mchezaji anaonekana anataka kupata nafasi, nao pia wanajua umuhimu wa hizi mechi.

"Tumekuwa na mazoezi mara mbili kwa siku, asubuhi wachezaji wanakwenda gym, jioni tunakwenda uwanjani, unajua kwa bahati nzuri tunacheza na timu ambayo tulikuwa nao kundi moja kwenye kufuzu AFCON kwa hiyo kwanza tunawajua vizuri, na bila shaka tunawafuatilia ambavyo inawezekana ili kujua walivyo, na sisi kuingia vipi kuwakabili," alitamba Morocco.

Kwa upande wa mshambuliaji wa Stars, Simon Msuva alisema mechi yao dhidi ya Niger haitakuwa rahisi kwa sababu timu hizo zinajuana na aliwahi kuwafunga bao 1-0.

Alisema wamekuja kufanya kazi kupambania taifa katika michezo hiyo miwili wakianza na Niger utakaochezwa Jumamosi kabla ya kuikaribisha Morocco Jumanne ijayo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# DSTV TANZANIA YATANGAZA RAHA YA MSIMU WA SIKUKUU

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kunogesha zaidi msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka na mwaka mpya, Kampuni ya MultiChoice Tanzania, imetangaza ofa kabambe kwa wateja wake na kwa wale wanaojiunga na huduma zao kupitia kampeni yake maalum inayokwenda kwa jina la 'Raha Mfululu na DStv'.

Kampeni hiyo ina lengo la kuhakikisha Watanzania wengi wanapata huduma hiyo ili waweze kufurahia burudani, elimu na habari wao na familia zao msimu huu wa sikukuu, ambapo mteja atapata kisimbuzi cha DStv kwa Sh. 59,000 tu na zawadi ya kifurushi cha Shangwe mwezi mmoja bila malipo ya ziada.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo juzi, Kaimu Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Semu Bandora, alisema wateja wao sasa watapata burudani zaidi za kusisimua kupitia soka, filamu, tamthilia, katuni na vipindi mbalimbali vya watoto vitakavyoileta familia pamoja na kuimarisha upendo.

**Aidha, Semu ameeleza kuwa mara kwa mara wamekuwa wakiwatunuku wateja wao wa zamani na wapya zawadi na ofa kabambe huku wakiendelea kupata burudani ya uhakika muda wote kwani kwa mwaka huu wamekua wakitoa mfululizo wa zawadi kwa wateja wote.**

Kwa upande wa Meneja Maudhui wa kampuni hiyo, Noel Mulumba, ameongeza kuwa katika msimu huu kumeongezwa maudhui 'kedekede' kwa wateja ikiwamo chaneli ya muda ya Sikukuu ya 'Holiday Pop Channel DStv 198', itakayoanza kuruka rasmi Ijumaa wiki hii hadi Januari 2, mwakani.

"Mbali na chaneli hii maalum, wateja wetu pia wataweza kufurahia tamthilia mpya za kinyumbani za 'Dhohar na Chanda' kupitia chaneli ya Maisha Magic Bongo, Ligi kubwa mbalimbali za soka zinazoendelea ulimwenguni ikiwamo Ligi Kuu ya Uingereza (EPL), LaLiga , Serie A, FA Cup, Carabao, UEFA Europa na nyinginezo.

"Kama haitoshi wapenzi wa soka wakae mkao wa kula kwani tumekuja na kipindi maalum cha uchambuzi wa mpira cha 'Supa Soka', kitakachokuwa kikiendeshwa na mwanahabari nguli Salim Kikeke sambamba na vipindi mbalimbali vya watoto ambao sasa wanaanza likizo vinavyopatikana ndani ya chaneli za Watoto kadha wa kadha ikiwamo 'Disney Junior, Cartoon Newtork' pamoja na 'Moonbug'," alisema Noel.

Uzinduzi huo pia uliambatana na kutambulishwa kwa wanafamilia wapya wa DStv ambapo wachekeshaji kama Mzee Shayo, Eliudi, Jol Master, Zulii Comedy, Mwanadada Zai Kijiwe Nongwa na She Is Lola, walitambulishwa rasmi kama wanafamilia wapya wa DStv Tanzania katika msimu huu wa sikukuu.




Mwanahabari nguli na mwanafamilia mpya wa DStv kupitia Kipindi cha Supa Soka, Salim Kikeke, akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni mpya ya "Raha Mfululu na DStv" uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## *Simba kwa Chasambi, Yanga kwa Chivaviro*

INATOKA UKURASA 24

risha dogo kazi itakayofanyika ni kuwataja na si kutafuta.

"Tayari benchi la ufundi chini ya Miguel Gamondi, limeshawasilisha ripoti kwa uongozi kwa maana ni maeneo gani yanatakiwa kufanyiwa marekebisho, ni aina gani ya wachezaji wanaotakiwa kuja kuiongezea nguvu timu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara, kuna Kombe la FA ambalo halijaanza na Kombe la Mapinduzi.

"Tunataka ikifika mzunguko wa pili, hawa watu tunaowaongeza na dozi ziongezeke siyo mabao matano tena, dirisha likishafunguliwa kazi yetu itakuwa ni kutangaza wachezaji na si kutafuta, tumeshazungumza na wachezaji tunaowahitaji kwa sababu hakuna muda wa kusubiri," alisema.

## Watuhumiwa watano Simba 5G

INATOKA UKURASA 24

Alisema wamepokea CV nyingi za makocha mbalimbali lakini wameweka vigezo vyao na tayari amepatikana, hivyo kinachosubiriwa ni muda wa kumtambulisha rasmi.

"Ni kweli tunahitaji kupata kocha mkuu kabla ya haya mapumziko ya Kalenda ya Fifa kufikia tamati, tungependa wiki ijayo tunapokwenda kwenye mchezo wa kimataifa dhidi ya Asec Mimosas tuwe tayari tumeshamtangaza kocha wetu," alisema Kajula.



Mtendaji huyo aliwataka mashabiki wa Simba kutulia na kuendelea kuunga mkono viongozi na wachezaji kuelekea maandalizi ya mchezo wao wa kimataifa dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast .

"Makocha walikuwapo wanaendelea na majukumu yao ya kukisuka kikosi kwa wachezaji wetu kujiandaa na mchezo huo kusaka ushindi na kutafuta alama tatu muhimu za nyumbani," alisema Mtendaji huyo.

Michezo
Jumatano Novemba 15, 2023
Nipashe




Fabregas kocha mpya Como UKURASA 22

## MTANZANIA ATUA BAYERN KWA BIL. 9/-




Winga Mtanzania Nestory Irankunda, akiwa na familia yake baada ya kusaini mkataba wa muda mrefu wa kuitumikia Bayern Munich ya Ujerumani akitokea Klabu ya Adelaide United ya Australia. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 17, ni mzaliwa wa Kigoma, Tanzania, ambaye kwa sasa anaitumikia Timu ya Vijana ya Australia na amesajiliwa kwa kitita cha pauni milioni 3 (Sh. bilioni 9 za Tanzania). Atajiunga na Bayern Julai 2024. **PICHA: MTANDAO**

# Simba kwa Chasambi, Yanga kwa Chivaviro

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## Ni katika kuimarisha vikosi vyao usajili wa dirisha dogo, Mtibwa, Kaizer Chiefs kubomolewa...

WAKATI dirisha dogo la usajili likitarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu, vigogo vya soka nchini ambavyo ni watani wa jadi, Simba na Yanga, tayari vimerusha ndoana zao kwa baadhi ya wachezaji ili kuimarisha vikosi vyao, na mambo yanakwenda bararaba kabisa, imeelezwa.

**Na kwa mujibu wa taarifa za uhakika kutoka ndani ya klabu hizo, zote zimeanza kwa kumulika katika kuimarisha safu zao za ushambuliaji, Simba ikitua kwa Kiungo Mshambuliaji wa Mtibwa Sugar na Taifa Stars, Ladeki Chasambi huku Yanga ikitua Afrika Kusini na kubisha hodi kwa Mshambuliaji wa Kaizer Chiefs, Ranga Chivaviro.**

Taarifa za uhakika zilizoifikia Nipashe jana, viongozi wa Klabu ya Simba wamekuwa katika mazungumzo na Chasambi na makubaliano ya awali na klabu yake yanaendelea huku nyota huyo akiwa tayari ameridhia kupewa mkataba.

"Ni kweli usajili umeanza kufanyika, Chasambi amekuwa katika mazungumzo na Simba bado yanaendelea kwa sababu wameshakubaliana kwa mkataba wa awali, huu usajili kwa upande wa mchezaji mzawa," alisema mtoa habari huyo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alipoulizwa alisema ni mapema kuzungumzia suala la usajili kipindi cha dirisha dogo hadi hapo tathimini ya kocha mkuu itakapofanyika.

"Kwa sasa hatuwezi kuongelea usajili wa dirisha dogo kwa sababu wachezaji tuliokuwa nao ni wazuri na suala la kuongeza nguvu kwenye kikosi litafanyika baada ya kufanyika tathimini na benchi la ufundi kuona wapi wanatakiwa kupaboresha," alisema Ahmed.

Nipashe lilimtafuta Mtendaji Mkuu wa Mtibwa Sugar, Swabri Aboubakar, lakini alisema yuko kwenye kikao cha bodi ya timu hiyo, hivyo atafutwe baadaye na hadi tunakwenda mitamboni hatukufanikiwa kumpata tena.

Kwa upande wa Yanga, taarifa za ndani za klabu hiyo zinasema, Chivaviro, ambaye msimu uliopita aliichezea Marumo Gallants ambayo ilikuwa kundi moja na Yanga katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, ni mmoja wa wachezaji wanaoweza kuongezwa kipindi cha dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 16, mwaka huu.

Straika huyo ilikuwa nusura atue Yanga baada ya msimu kumalizika, lakini aliibukia Kaizer Chiefs, huku taarifa zikisema kwa sasa hana furaha kwenye kikosi hicho kwa kukosa namba ya kudumu, hivyo klabu yake inaweza kukubali kumuuza au kumtoa kwa mkopo.

Taarifa zinasema kuwa moja ya sababu za Injinia Hersi Said kwenda Afrika Kusini, pamoja na mambo mengine ni suala ya usajili wa baadhi ya wachezaji, akiwamo mchezaji huyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jana kuwa tayari faili la Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, limetua kwa viongozi chini ya Injinia na sasa linafanyiwa kazi.

Bila kutaja wachezaji ambao itawasajili au nafasi zao wanazocheza uwanjani, Kamwe alisema tayari viongozi wameshazungumza na wachezaji inaowahitaji na itakapofika di-

INAENDELEA UKURASA 23

# Watuhumiwa watano Simba 5G wapelekwa kwa Kova

**Na Saada Akida**

NYOTA watano wa Simba waliokuwa kikaangoni baada ya mechi ya Yanga, sasa wamepelekwa kwenye kamati ya nidhamu inayoongozwa na Kamishna wa Polisi wa zamani wa Mkoa wa Dar es Salaam, Suleiman Kova.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya nyota hao kudaiwa kuihujumu timu kwenye mchezo wa 'Kariakoo Derby' dhidi ya Yanga na kusababisha kufungwa mabao 5-1, Novemba 5, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Iman Kajula, alisema Simba haifanyi jambo kwa kukurupuka na kila sehemu ina kamati mbalimbali ikiwamo uchunguzi na nidhamu.

Alisema katika fununu zilizotolewa kuhusu wachezaji hao, linafanyiwa kazi na kupelekwa kwenye kamati ya nidhamu ambayo inawajibu kufanyia kazi na kutoa hukumu pale ambapo kuna bainika kuna makosa.

"Zile fununu au tetesi za nyota hao tayari zinafanyiwa kazi na kamati itakuja kutolea majibu endapo itabainika kuna makosa, viongozi watatekeleza kwa kuchukuwa hatua," alisema Kajula.

Aliongeza: "Klabu ya Simba tunaamini kupiga hatua kubwa katika maendeleo ya michezo lazima kuwapo nidhamu sifa ya kwanza kwa mchezaji uongozi hawatafumbia macho mchezaji au mwajiriwa ndani ya klabu hii anayeonesha utovu wa nidhamu."

Alisema lazima mchezaji au mwajiriwa ndani ya klabu hiyo atahukumiwa kulingana na jambo ambalo amelifanya pindi uchunguzi wa kina na kamati ya nidhamu zitakapojiridhisha.

Kuhusu mrithi wa Robertinho Oliveira, Kajula alisema mchakato unaendelea na siku chache zijazo watamtangaza kocha mkuu pamoja na wa viungo.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >